# Nipashe

Jumatatu Novemba 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580401

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ    nipasheTZ    nipasheTZ    0745 700710





UKURASA 11

**MIAKA 30** jela kwa unyang'anyi wa silaha

UKURASA 4



**MAASKOFU** CPCT watoa tamko uchaguzi mkuu

UKURASA 2

# Watajwa kurejea Baraza la Mawaziri



William Lukuvi



Jenister Mhagama



Prof. Joyce Ndalichako



Selemani Jafo



Ummy Mwalimu

**NI** wakati huu ambao Rais Magufuli anasubiriwa kulitangaza...*Endelea Uk. 2*




Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, wakati wa hafla ya kuwapongeza wabunge iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ma-RC watoa angalizo kupanda bei ya saruji

UKURASA 8

## Marekani kujenga viwanda korosho

UKURASA 3

**MICHEZO** MSUVA: WYDAD NJIA YA KUNIPELEKA ULAYA UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Maaskofu CPCT watoa tamko la uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Maaskofu wa makanisa ya kipentekoste nchini (CPCT), limewataka Watanzania kuwa watulivu na kuwapa nafasi viongozi waliochaguliwa kutekeleza wajibu wao na kuleta maendeleo kwa taifa.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Askofu Peter Konki, aliyasema hayo jana alipokuwa akisoma tamko la baraza hilo kwa waandishi wa habari.

"Baraza la Maaskofu lina sababu ya kumshukuru Mungu, kwa zawadi hii na kwa namna anavyoilinda nchi yetu na kuifanya tulivu baada ya uchaguzi mkuu...tunatoa wito kwa kila mmoja wetu kuendelea kumwomba na kumshukuru Mungu ili aendelee kulitunza taifa na viongozi wetu," alisema Askofu Konki.

Alisema baraza hilo linawapongeza Watanzania wote, kwa kuwa watulivu wakati wote wa kampeni, kupiga kura na kupokea matokeo.

"Kwa vile viongozi wameshapatikana tunatambua juhudi za kila Mtanzania katika kutunza utulivu na umoja wetu tutoe wito kwa kila raia kuwa mtulivu na kuwapa nafasi viongozi waliochaguliwa kutekeleza wajibu wao na kuleta maendeleo kwa taifa," alieleza Askofu Konki.

Aidha, alisema pia baraza linatoa pongezi kwa Rais John Magufuli kuchaguliwa tena kuliongoza Taifa la Tanzania pamoja na Makamu wake, Samia Hassan Suluhu na Dk. Hussen Ali Mwinyi kuwa Rais wa Zanzibar.

"Baraza la Maaskofu linaipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuandaa na kusimamia uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani kwa weledi na uwazi," alisema askofu huyo.

Hata hivyo, alisema baraza hilo linaiomba serikali kuendelea kupanga na kusimamia ukuaji wa uchumi katika kila sekta, ili kuondoa umaskini wa kipato na kuhakikisha kuwa uvunaji wa rasilimali za nchi unawanufaisha Watanzania wote.

Alisema, Baraza la Maskofu lina imani kubwa na Rais Magufuli na Dk. Hussen Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar kuwa wataongoza kwa uaminifu na haki na watalinda amani na umoja.



Meneja Mawasiliano wa TBL Plc, Amanda Walter (kulia), akifanya majaribio ya kuuzima moto wakati wa mafunzo ya kuukabili moto na majanga yaliyoandaliwa na kampuni hiyo, yaliyofanyika katika kiwanda cha Ilala mwishoni mwa wiki, (kushoto) ni Sajenti Katonga Omary wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watabiriwa kurudi Baraza la Mawaziri

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA zimepita siku 11 tangu kuanza kazi rasmi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi chake cha pili, majina ya baadhi ya waliokuwa mawaziri na manaibu katika kipindi cha kwanza, walioonyesha kuzimudu wizara zao, yametabiriwa na wananchi kurudi katika baraza jipya.

Baada ya kuapishwa Novemba 5, Rais John Magufuli na Makamu wake, Samia Hassan Suluhu, kwa kipindi kingine cha miaka mitano, alimteua Adelardus Kilangi, kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akiwa ni kiongozi wa kwanza wa ngazi za juu kurudi katika nafasi yake ya awali.

Rais Magufuli pia alimteua tena Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuendelea na wadhifa huo na kupata kura zote za ndiyo za wabunge wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano.

Alhamis, Novemba 12, aliwateua Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamaganda Kabudi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kuendelea na wizara yake.

Vile vile, alimteua Dk. Philip Mpango, kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, wizara ambayo aliishika katika kipindi cha kwanza cha serikali ya awamu ya tano.

Mawaziri ambao walianza na kumaliza na Rais Magufuli kwa kipindi cha kwanza ni aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anayetajwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kurudi katika nafasi hiyo.

Ummy alichaguliwa kuwa mbunge mpya wa Jimbo la Tanga Mjini kutoka ubunge wa viti maalum, katika awamu iliyopita.

Jina la Ummy linatabiriwa na wananchi wengi kutokana na utendaji na umahiri wake aliouonyesha katika wizara hiyo, hasa kipindi cha janga la corona.

Mwingine anayetabiriwa kurudi katika wizara yake ni Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ismani na Naibu wake, Angelina Mabula, Mbunge wa Jimbo la Ilemela.

Lukuvi, anatabariwa kutokana utendaji wake wa ufuatiliaji na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Aliyekuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ambaye ni Mbunge wa Kisarawe, Selemani Jafo, ambaye alianza kama Naibu Waziri na baadaye kupanda na kuwa waziri kamili, pia anatabiriwa kurejea tena katika wizara hiyo.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Jennister Mhagama na Naibu wake, Anthony Mavunde, ni kati ya mawaziri wanaopewa nafasi ya kurejea kwenye wizara hiyo.

Wengine wanaotajwa kubaki ni manaibu waziri ambao wamedumu kwenye Baraza la Mawaziri tangu walipoteuliwa mwaka 2015, ambao ni aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kondoa, Ashatu Kijaju, aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini, Prof. Joyce Ndalichako na aliyeanza kama Naibu Waziri wa Elimu mwaka 2015 na kumaliza kama Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya na Mbunge wa Jimbo la Nyasa.

Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano, ambaye alianza kama Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, na Mbunge wa Jimbo la Katavi, Issack Kamwele, pia anatajwa kuwa kwenye nafasi ya kubaki kwenye baraza hilo.

Miongoni mwa mawaziri na manaibu walioanza na kumaliza kwa nafasi zao ni Lukuvi, Mwalimu, Prof. Ndalichako, Mhagama, Mavunde na Mabula.

Akizungumza Ikulu Chamwino, Dodoma, wakati akimwapisha Mwanasheria Mkuu, Rais Magufuli, aliwataka watendaji wa umma kutulia na kufanya kazi kwa kuwa hatabadilisha, bali itakapolazimu kama watashindwa kufanyakazi vizuri au kuacha wenyewe.

Alisema kwa mawaziri na manaibu, atabadilisha kwa kuwa anao wengi wanaotokana na wabunge wa Bunge la 12 ambao kwa CCM ina jumla ya wabunge 264 wa majimbo na viti maalum 94. "Mabadiliko yatakayokuwapo ni kwenye nafasi za uwaziri ambazo tulienda kuomba kura wote, hizo lazima tutabadilisha, wapo watakaorudi, wapo ambao hawatarudi tena siku hizo zipo 'option' (nafasi) ni kubwa nina wabunge 264 kwa hiyo uchaguzi ni mkubwa zaidi sitaki kusema uongo, nikishamaliza hivyo basi wengine wachape kazi tu," alisema.

## ANATAFUTWA



SIMON MAKOYE .........ANAYEONEKANA KWENYE PICHA HAPO JUU ANATAFUTWA NA POLISI KWA TUHUMA YA WIZI WA KUAMINIWA. YEYOTE ATAKAYEMUONA POPOTE TAFADHALI TOA TAARIFA KWA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU YAKO.

POLISI TAARIFA **OB/RB/5063/2020**

## ENEO KUBWA LINAUZWA BAHARI BEACH

LIPO BARABARA YA NYOTA NJEMA, BAHARI BEACH, KUNDUCHI DAR ES SALAAM. UKUBWA 5,557 SQ. MTS (EKA MOJA NA ROBO). KUNA NYUMBA YA WAGENI VYUMBA 2 SELF CONTAINED NA KUNA NYUMBA YA MLINZI. MAJI NA UMEME UPO. ENEO LOTE LIMEZUNGUSHIWA UKUTA WA MATOFALI.

**WASILIANA SIMU NA. 0655350954**

115994902

## HABARI KITAIFA

# Anusurika kifo kwa kutumbukia shimo la choo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Mtaa wa Nyanza, Kata ya Kalangalala, Butogwa Daudi (22), amenusurika kifo baada ya kutumbukia kwenye shimo la choo lenye urefu wa futi 25 na kuokolewa na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Zabrone Muhumha, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 3:49 asubuhi.

Muhumha alisema chanzo cha kutumbukia kwenye shimo hilo kwa mujibu wa mama mzazi, Reema Jumanne (45), alimwagiza binti yake Butogwa kutoa godoro nje na yeye akawa anaendelea kufua nguo.

Alisema alipotoka nje akakuta godoro na kuona kandambili alizokuwa amezivaa binti yake huyo na aliposogea karibu na shimo hilo na kuchungulia ndani alimuona binti yake amesimama ndani.

"Sisi askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji tulipewa taarifa kutoka kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Geita na baada ya kupata hizo taarifa askari wa Jeshi la la Zimamoto na Uokoaji tulienda eneo la tukio na tulipofika, tukakuta binti huyo yumo ndani ya shimo la choo tulipanua tundu tukaingiza ngazi ndani na tukafanikiwa kumwokoa binti huyo akiwa mzima," alisema.

Alisema baada ya kutolewa ndani ya shimo aliogeshwa na kupelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita kwa uchunguzi zaidi. Baba mzazi wa binti huyo, Jumanne Sizya, alisema binti yake alifikishwa hospitali na kufanyiwa uchunguzi na kukutwa hali yake ni nzuri na kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Sizya alisema anamshukuru Mungu kwa sababu maji machafu kwenye shimo hilo yalikuwa machache, yangekuwa mengi mtoto wake angefariki dunia.

Pia, aliwashukuru askari wa Zimamoto na Uokoaji kuwahi kufika kwenye eneo la tukio na kumwokoa binti yake.

# Marekani kuwekeza viwanda vya korosho

**Na Said Hamdani,** LINDI

KAMPUNI ya Ward Holdings Internaizomal (WHI) ya Marekani imeonyesha nia ya kuwekeza ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho.

Viwanda hivyo vinavyoelezewa kuwa ni vya kisasa, vitajengwa Manispaa ya Lindi mkoani Lindi, Mtwara na Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, na ujenzi unatarajiwa kuanza mwakani.

Hayo yalibainishwa na mwakilishi wa WHI anayeshughulikia pia masuala ya uwekezaji na masoko upande wa Afrika, Godfrey Simbeye,(pichani), katika mahojiano maalumu na Nipashe.

Simbeye na ujumbe wake walifika mkoani Lindi kuwasilisha rasimu ya makubaliano namna ya ushirikiano kati ya uongozi wa WHI, Manispaa na Umoja wa Wakulima wa Korosho (TARUCHINA) kuhusu uwendeshaji wa kiwanda hicho.

"Hiki kiwanda kitapoanza kufanya kazi rasmi, kitakuwa na uwezo wa kubangua tani 20,000 za korosho kwa mwaka," alisema Simbeye.

TARUCHINA ni muunganisho wa wakulima wa korosho kwa vijiji vinne vinavyojishughulisha pia na ulimaji korosho, Tandangongoro, Ruaha, Chikonji na Nandambi.



Alisema (TARUCHINA) ndio watakuwa wamiliki wakuu wa kiwanda hicho, ambapo WHI na wadau wengine watachangia fedha kwa ajili ya ujenzi wake, huku akiusisitiza uongozi wa Umoja kuongeza kasi ya uzalishaji wa korosho kulisha kiwanda hicho.

Mwenyekiti wa Kampuni hiyo, Lloyd Ward Ceox, alisema ujenzi wa kiwanda cha Lindi pekee utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.5 hadi kukamilika kwake, wakati kazi ya ujenzi itaanza rasmi Juni mwakani.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Batsta Kihanz, alisema wameshawapatia eneo la ukubwa wa ekari tatu maeneo ya Ngongo na iwapo watahitaji zaidi, watawaongezea kukamilisha hitaji lao.



# Waenda jela miaka 30 kwa unyang'anyi kutumia silaha

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita Mkoa wa Geita imewahukumu watu watatu wakazi wa Kijiji cha Busanda mkoani Geita kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la unyang`anyi wa kutumia silaha.

Waliohukumiwa ni Petro Mlongo (29), Masumbuko Sakumi (25) na Jackson Masumbuko (26) wote wakazi wa Kijiji cha Businde Wilaya ya Geita.

Wote hao wamehukumiwa baada ya kukutwa na hatia ya kutumia panga kumjeruhi Zwiyo Mpemba kichwani na mkononi na kumpora Sh. 300,000 pamoja na simu mbili aina ya Nokia na nyingine aina ya Itel, zote zikiwa na thamani ya Sh. 120,000.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo.

Hakimu Kiiza alisema mahakama hiyo imetoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa vijana wengine wenye tabia za kikatili kama hizo.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo alipeleka hapo mahakamani mashahidi 8 na vielelezo 4 ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo.

Alidai Julai 14 mwaka 2014 usiku katika Kijiji cha Msasa mkoani Geita mlalamikaji Zwiyo Mpemba akiwa amelala nyumbani kwake, alivamiwa na washtakiwa hao wakiwa na panga na kumwamuru atoe fedha pamoja na simu alizokuwa nazo.

Aliieleza mahakama kuwa baada ya mlalamikaji huyo kukataa kutoa fedha na simu, washtakiwa hao walimcharanga na mapanga kichwani na mkononi na hivyo kumlazimu kutoa fedha kiasi hicho cha fedha cha Sh. 300,000 na simu mbili.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa adhabu yao, waliangua vilio huku wakiiomba mahakama hiyo iwapunguzie adhabu kwa kuwa ni kosa lao la kwanza na wanategemewa na wazazi.

Hakimu Kiiza alitupilia mbali utetezi huo na kusema washtakiwa wote kwa pamoja ni vijana wenye nguvu.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, akizungumza na wafanyakazi wa NBC pamoja na wafanyabiashara wadogo wa wilaya hiyo, wakati benki hiyo ilipozindua huduma mpya ijulikanayo 'NBC Kua Nasi'. Huduma hiyo inawawezesha wajasiriamali kuweka akiba ya pesa za mauzo kwa unafuu na usalama zaidi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lowassa aongoza harambee ujenzi jengo la KKKT

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, ameongoza harambee ya kuchangia ujenzi wa jengo la makao makuu ya Dayosisi ya Kaskazini Kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), linalojengwa jijini Arusha kwa gharama ya Sh. bilioni 11.

Katika harambee hiyo, Lowassa alifanikiwa kuchangisha Sh. milioni 326.5

Kati ya fedha hizo, fedha taslimu ni Sh. milioni 152.7 na ahadi ni Sh. milioni 173.8

Akizungumza wakati wa harambee hiyo iliyowashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi na wafanyabiashara, Lowassa aliwataka Watanzania kuendelea kujenga misingi na mazoea ya kuchangia miradi yao ya maendeleo na kuachana na dhana ya kutegemea wahisani. Aidha, Lowassa alisisitiza umuhimu wa wananchi kujitolea kujenga na kuboresha nyumba za ibada ili ziweze kuwa kivutio cha watu kumwomba Mungu hatua ambayo ina tija kubwa kwa maisha ya kila siku ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Suala la watu kujitolea kuchangia maendeleo yao halina mbadala wake na lina tija kubwa na ndio maana hata Rais wetu, Dk. John Magufuli, anasisitiza watu wafanye kazi kwa bidii, pia kujitolea kwa ajili ya Mungu na kuna faida nyingi na kubwa," alisema Lowassa.

Katika harambee hiyo, Lowassa alichangia Sh. milioni 10.

Kabla ya harambe hiyo, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Solomoni Masangwa, alisema ujenzi wa jengo la kisasa la makao makuu ya dayosisi hiyo ni mpango ulioanza mwaka 2014.

Aidha, Askofu Masangwa alisema ujenzi wake unalenga kuimarisha utoaji wa huduma unaoweza kukidhi mahitaji na kwenda na wakati.

"Unajua Arusha ni mji wenye sifa kubwa kitaifa na kimataifa.

"Kwanza ni makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, pia katikati ya Afrika na mji wa kitalii. Sasa kwa hizo sifa chache ni dhahiri kwamba lazima tuwe tayari kwa kila hali kuhudumia watu kutoka mataifa mbalimbali na ili malengo yatimie lazima tuboreshe miundombinu," alisema Askofu Masangwa.

Kwa mujibu wa Askofu Masangwa, ujenzi wa jengo la cathedral hiyo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 11 na litakuwa sehemu mbalimbali za kutolea huduma ikiwamo ya kufanyia ibada yenye uwezo wa kubeba waumini 1,700.

Pia litakuwa na jengo la utawala na litakuwa na ghorofa mbili, na eneo la kuegesha idadi kubwa ya magari zaidi ya 270.

"Mara nyingi wote tumewona mheshimiwa Lowassa akiwa mstari wa mbele kuhamasisha na pia kushiriki kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya kujenga nyumba za ibada kwa madhehebu yote, kwa kweli ni mfano wa kuigwa na viongozi wengine na pia kwa Watanzania wote," alisema Askofu Masangwa.

Katika harambee hiyo wadau mbalimbali walishiriki wakiwamo viongozi wa serikali, mashirika, sekta za umma na binafsi akiwamo mkurugenzi wa TAHA, Dk. Jackline Mkindi, ambaye alisema suala la kuimarisha nyumba za ibada linapashwa kuwa endelevu kwani kuna umuhimu mkubwa wa kila mtu kufanya ibada.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa kamati ya maendeleo wa kanisa hilo, Darius Bipa, mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo ameshapatikana na linajengwa na Kampuni ya Elerai Construction Ltd.

## RITA yaanzisha kitengo cha kuandika wosia

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), umeanzisha kitengo cha kuandika na kuhifadhi wosia baada ya kuonekana kwa tatizo kwenye usimamizi wa mirathi katika familia.

RITA huteuliwa na mahakama kusimamia mirathi wakati wanufaika wanaposhindwa kuelewana.

Kwa mujibu wa RITA, wosia ni tamko analolitoa mtu wakati wa uhai wake akieleza mahali atakapozikwa na jinsi anavyotaka mali yake igawanywe au watu aliowateua kupewa baada ya kifo chake.

"Huduma ya kuandika na kuhifadhi wosia ilianzishwa na wakala mwaka 2008 na mpaka sasa jumla ya wosia 723 zimeandikwa na kuhifadhiwa RITA. Takwimu hii inaonyesha ni jinsi gani jamii inavyozidi kuelimika kuhusu kuandika na kuhifadhi wosia," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na RITA.

Akiongelea umuhimu wa kuandika wosia katika maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria mkoani Tanga, Mwanasheria wa Serikali Mwandamizi kutoka RITA, Janeth Mandawa, alisema: "Watanzania wengi wamekuwa na mawazo potofu juu ya kuandika wosia, wengi wao wakiamini ni sawa na kujichulia kifo cha mapema jambo ambalo halina ukweli wowote, kwasababu kitendo cha kuandika wosia ni suala la kisheria na lenye faida kubwa inapokuja usimamizi wa mirathi ya familia," alisema.

Alitaja faida za kuandika wosia kuwa ni kuepusha watoto, mke au mume kunyang'anywa mali, kumwezesha kumchagua msimamizi wa mirathi, kuepusha migongano na migogoro katika familia.

Vile vile, wosia unampa uhakika wa maisha bora ya baadaye ya mrithi kulingana na mali alizonazo mtu, hupunguza gharama na usumbufu wakati wa kuendesha mirathi.

"Huduma hii ya kuandika na kuhifadhi wosia hutolewa katika Ofisi za RITA makao makuu, Dar es Salaam pamoja na Ofisi ya Kanda Dodoma na wanasheria wa serikali waliobobea katika masuala ya wosia na mirathi na hutunzwa kwa umakini na usiri mkubwa," alisema.

Alifafanua kuwa gharama za kuandika na kutunza wosia ni nafuu.

Akitoa ushauri kwa jamii, Mandawa alisema wananchi lazima watambue kuwa ni jambo zuri na muhimu kwa mtoa wosia kuandaa maisha bora ya warithi wake akiwa bado hai utakaosaidia kutoa mwelekeo wa mgawanyo halisi wa mali za muhusika na hivyo kusaidia pia kuondoa au kuzuia migogoro katika familia.

Alisema RITA inaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kupitia vyombo vya habari, mikutano ya wadau pamoja na mitandao ya kijamii kuifikia jamii kwa ukaribu zaidi ili iweze kufaidika na huduma zitolewazo na wakala huyo. Pia RITA imeanzisha kituo maalum cha huduma kwa wateja kwa kupiga simu kwa namba 0800117482 bila gharama.

# Dk. Tulia aipa NMB siri ya kuzalisha mabilionea wengi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA



NAIBU Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, (pichani), ameishauri Benki ya NMB, kuwezesha wawekezaji wazalendo ili kutimiza azima ya Rais John Magufuli ya taifa kuwa na mabilionea wengi.

Dk. Tulia aliyasema hayo juzi wakati wa hafla iliyoandaliwa na benki ya NMB, kwa wabunge wote wa Bunge la 12, lililozinduliwa hivi Ijumaa na Rais Magufuli.

Alisema pamoja na mafanikio mengi iliyoyapata, benki hiyo pia inatakiwa kuwezesha wawekezaji wazalendo, kwa kuwapatia mikopo ambayo itasaidia kuwainua kibiashara.

"NMB inatakiwa hivi sasa kuwawezesha wawekezaji wazalendo, ili wale mabilionea mheshimiwa Rais aliokuwa akiwasema wakati wa hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge la 12, iweze kufikiwa," alisema Dk. Tulia.

Aidha, alisema NMB inao uwezo wa kuwashawishi wawekezaji wazalendo na kuwasaidaia kuinua eneo la uwekezaji.

Vile vile, Dk. Tulia aliipongeza benki hiyo kwa kuendelea kuboresha huduma zake na kujitanua kiutendaji katika kila eneo nchini.

"Niwapongeze NMB, kwa kazi zenu mnazozifanya nimesikia hivi sasa mnamiliki mali za trilioni saba, hii inaonyesha kuwa ni kwa kiasi gani fedha zetu zipo salama kwenu," alieleza.

Pia, aliipongeza benki hiyo, kwa gawio ambalo imekuwa ikitoa kwa serikali ili kusaidia kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo.

Dk. Tulia alisema kutokana na benki hiyo kuja na huduma ya bima ya afya kwa kushirikiana na mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF) utakuwa mkombozi kwa afya za Watanzania.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipua, alisema hivi sasa wanaondoka katika mfumo wa uuzaji bidhaa na kuleta suluhisho katika jamii.

Zaipuna, alisema wanatoa huduma ya bima ya afya kwa jamii inayoenda kwa jina la dunduliza inayomsaidia mtu kujikusanyia fedha na kulipia bima yake.

"Utaratibu huu unamwezesha Mtanzania kujikusanyia kiasi cha fedha, ili kulipia bima yake kwa mwaka katika mfuko wa bima ya afya wa taifa NHIF, kidogo kidogo ili kuwa na uhakikia wa matibabu," alieleza Zaipuna.

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, aliwapongeza wabunge wote waliochaguliwa katika Bunge la 12 na kuwataka kujivunia benki hiyo ambayo kwa asilimia kubwa inamilikiwa na serikali ya Tanzania.

## Kizimbani tuhuma za kuharibu mali

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wanne wa Kijiji cha Chiumbati, Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, wamefikishwa mahakama ya mkoa huo, wakikabiliwa na kosa la kuharibu mali kwa makusudi na kusababisha hasara ya Sh. milioni 3.4, mali ya ofisi ya Serikali ya Kata.

Washtakiwa hao ni Juma Selemani Mkumila (39), Daila Abdallah Maulidi (46), Salum Said Duwa (30) na Ally Said Bakari (27), na kusomewa shtaka na Mwanasheria wa Serikali, Abdurahamani Mohamedi.

Mohamedi alitaja mali zinazodaiwa kuharibiwa ni viti/ mabenchi ya kukalia 10, meza tatu na kabati moja, vyote vikiwa na thamani ya kiasi hicho cha fedha, mali ya ofisi ya Kata ya Chiumbati, wilayani Nachingwea.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Elimo Massawe, Mwanasheria Mohamedi alidai washtakiwa wanadaiwa kufanya uharibifu huo, Novemba 28, mwaka huu, majira ya usiku.

Alidai kwamba kutokana na kitendo hicho cha kuharibu mali, washtakiwa wamefanya kosa kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 326 (1) kanuni ya adhabu sura ya 16 ya mwaka 2019.

Washtakiwa wote walikana kosa na kupelekwa mahabusu. Kesi yao namba 24/2020, imepangwa kutajwa tena kesho.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars msirudie makosa ya Tunisia kwa Mkapa kesho

**KESHO** timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuikaribisha timu ya Taifa ya Tunisia katika mechi ya marudiano ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022, zitakazofanyika nchini Cameroon.

Mechi hiyo ni ya nne kwa Stars kwenye Kundi lao la J, lakini ikiwa ni ya marudiano dhidi ya Watunisia hao baada ya Jumamosi iliyopita kukubali kipigo cha bao 1-0 ikiwa ugenini, hivyo kujikuta inapoteza mechi yake ya tatu hadi sasa.

Katika kundi hilo la J, ambalo Tunisia ipo kileleni ikiwa na pointi tisa baada ya kushinda mechi zote tatu, Stars inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama tatu sawa na Equatorial Guinea na Libya inayoburuza mkia kutokana na kuruhusu mabao mengi ya kufungwa.

Equatorial Guinea ipo nafasi ya pili kutokana na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa, hivyo ushindi kwa Stars kesho utaifanya kukalia nafasi hiyo ya pili na kujiweka katika sehemu nzuri ya kufuzu michuano hiyo kwa mara ya tatu katika historia yake.

Huo utakuwa mchezo wa pili kwa Stars kucheza nyumbani baada ya ule wa awali dhidi ya Equatorial Guinea kushinda 2-1 na kisha kwenda ugenini na kujikuta nayo ikiangukia kipigo kama hicho dhidi ya Libya kabla ya wiki iliyopita kuchapwa bao 1-0 na Tunisia.

Tunatambua haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande hasa kutokana na ubora wa Tunisia, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu kwa Stars kushindwa kupata matokeo nyumbani mbele ya mashabiki wake takriban 30,000 watakaoruhusiwa kushuhudia mechi hiyo.

Tunaamini kama Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije atakuwa amefanyia kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika mchezo uliopita, Tunisia inaweza kujikuta ikishindwa kufua dafu katika mechi hiyo ya marudiano ambayo kwa Stars uwanjani itakuwa na mchezaji wa 12, ambao ni mashabiki.

Wote tunatambua umuhimu wa kucheza nyumbani mbele ya mashabiki wako, jambo ambalo Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) limeruhusu asilimia 50 ya mashabiki kuhudhuria mechi hiyo kesho, tofauti na Tunisia ambayo kwao ilizuiwa kutokana na janga la virusi vya corona kuendelea kuliandama taifa hilo.

Hivyo, kwa Uwanja wa Mkapa ambao huchukua mashabiki 60,000, ni nusu yake tu watakaoruhusiwa kuhudhuria mechi hiyo inayotarajiwa kuwa na ushindani mkali kutokana na Tunisia nayo kutaka kujihakikishia kufuzu mapema na ili kuziacha, Tanzania, Equatorial Guinea na Libya zikiwania nafasi moja katika kundi hilo.

Aidha, wakati tukiamini benchi la ufundi limefanyia kazi makosa yaliyowafanya kukosa ushindi kwenye mechi hiyo ya awali, huku wachezaji nao wakijipanga kulipa kisasi nyumbani, jukumu lililobaki ni kwa mashabiki kutumia fursa hiyo ya kuruhusiwa kushuhudia mechi kwa kwa kujitokeza kwa wingi kesho kuishangilia Stars.


Tuaamini kama mashabiki 30,000 watajitokeza kesho na kuishangilia Stars mwanzo mwisho, watasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza hamasa kwa wachezaji na hatimaye kujituma zaidi, hatimaye kupata ushindi.

Lengo letu ni kuona Stars inapata ushindi mechi zote za nyumbani kwani baada ya mchezo huo itakuwa imebakiza mmoja katika Uwanja wa Mkapa dhidi ya Libya na dhidi ya Equatorial Guinea kwao.

Hivyo, kuvuna pointi tisa nyumbani na kisha kujipanga angalau kwenda kuambulia pointi moja ugenini dhidi ya Equatorial Guinea, kutakuwa kumeifungulia njia Stars ya kwenda Cameroon kushiriki michuano hiyo mikubwa kabisa barani Afrika.

Hatutarajii kuona wachezaji Stars wakirudia makosa waliyoyafanya katika mchezo uliopita jijini Tunis, Tunisia na badala yake tunataka kuona kila mmoja akionyesha thamani ya kuvaa jezi ya taifa kwa kuipambania mwanzo mwisho hadi kuibuka na ushindi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Suala la Senzo tuliache kwa vyombo vya dola kwanza

**AWALI** tulisikia habari za kukamatwa kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa Klabu ya Simba, Hashim Mbaga.

Moja kati ya tuhuma zilizotajwa ni kuihujumu klabu hiyo kongwe nchini Tanzania. Mbaga alikamatwa ikiwa ni miezi michache baada ya kusimamishwa kazi na uongozi wa klabu ya Simba.

Ikadaiwa kuwa aliachishwa kazi kutokana na kuwa na ukaribu na aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa raia wa Afrika Kusini. Mbaga aliachishwa kazi, wiki kadhaa baada ya Senzo kuandika barua rasmi ya kuacha kazi kwenye klabu hiyo.

Hivi majuzi, mashabiki wa soka nchini walipatwa na mshtuko baada ya Senzo kukamatwa kwa muda kabla ya kuhojiwa na Jeshi la Polisi na kuachiwa. Alishikiliwa kwenye kituo cha Oysterbay jijini Dar es Salaam kwa kile kinachodaiwa kuwa ni upangaji matokeo. Hata hivyo, aliachiwa baadaye, lakini habari zinadai kuwa uchunguzi bado unaendelea.

Taarifa zingine zinadai kuwa tuhuma zake ni za kuihujumu klabu yake ya zamani ya Simba. Kwa sasa Senzo akiwa mmoja wa maofisa wa klabu ya Yanga, kwa cheo cha Mshauri Mkuu wa Klabu kwenye masuala ya uwekezaji. Ingawa haiwekwi wazi sana, lakini inavyoonyesha mlalamikaji, au aliyepeleka kesi hii polisi ni klabu ya Simba.

Klabu zote mbili zimetoa taarifa zao kuhusu jambo hilo. Yanga ikilalamika na kudai kuwa hiyo ni nia ovu ya kumchafua Senzo mwenyewe na kuichafua taswira ya klabu yao.

Taarifa ya Yanga, inasisitiza kuwa masuala ya mpira wa miguu yanashughulikiwa na taasisi zinazohusika na usimamizi wa mpira wa miguu na si vinginevyo. Kwa upande wa klabu ya Simba ilitoa taarifa kuwa itatoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vya dola kuhusu tuhuma hizo.

Kumekuwa na maoni mbalimbali kuhusiana na tukio hili. Kila mmoja akisema lake. Wachambuzi nao kila mmoja akiongea vyake. Kuna waliotaka jambo hili lishughulikiwe na mamlaka za michezo. Wengine wanataka Jeshi la Polisi lishughulikie suala hili.

> **Klabu zote mbili zimetoa taarifa zao kuhusu jambo hilo. Yanga ikilalamika na kudai kuwa hiyo ni nia ovu ya kumchafua Senzo mwenyewe na kuichafua taswira ya klabu yao. Taarifa ya Yanga, inasisitiza kuwa masuala ya mpira wa miguu yanashughulikiwa na taasisi zinazohusika na usimamizi wa mpira wa miguu na si vinginevyo.**

Lakini ikumbukwe kwa muda mrefu sana kumekuwa na tuhuma za kupanga matokeo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mechi zingine hata kabla Senzo hajaja nchini.

Minong'ono na dhana hii imekuwa ni ya muda mrefu sana, hadi baadaye ikaonekana kama ni moja tu ya maisha kwenye soka la Tanzania.

Tuhuma hizi zilipelekwa hata kwenye mamlaka zinazoendesha soka la Tanzania. Lakini mara zote hazipati majibu ya kuridhisha. Majibu ya kuridhisha si lazime isemwe kuwa kuna rushwa. Hata taarifa rasmi tu itoke kuwa uchunguzi umeonyesha kuwa hakukuwa na tuhuma zozote. Matokeo yake mambo yanabaki kimya. Inawezekana kabisa tatizo likawa ni ushahidi. Na hili ndiyo tatizo kubwa kwenye soka la Tanzania. Ama ni ngumu sana kupata ushahidi, au wanaofanya michezo hii ni wajanja sana kiasi cha kushindwa kuacha alama za ushahidi nyuma.

Mimi nadhani suala la Senzo, sasa liachiwe kwa Jeshi la Polisi kwanza lifanye kazi yake. Ninavyojua jambo linalopelekwa polisi huwa na ushahidi. Inaonekana waliopeleka huko wana ushahidi wa kutosha, hivyo kusababisha rushwa ambalo ni kosa la jinai.

Lakini kupeleka ushahidi ni jambo moja na ushahidi huo kutosheleza kwenye kesi ni jambo lingine.

Hivyo, unaweza kupelekwa ushahidi, lakini kumbe si halisi, hivyo Senzo akawa huru na akaweza kushtaki ili kulipwa fidia kwa kuchafuliwa jina lake kama jambo hili linakwenda mahakamani.

Kama ushahidi utatosheleza, basi Tanzania inaweza kupata mwarobaini wa kulisawazisha soka letu ambalo hata wadau wenyewe wanakiri kuwa lina makandokando mengi.

Muhimu ni kwamba, tuliachie Jeshi la Polisi kwa sababu lenyewe lina Wataalamu, ndiyo watakaokuja kutuambia ukweli wote kama ni kweli au la, badala ya sisi kuongea na kuandika kwa kudhanidhani tu.

# Wananchi wapewa fursa kuondokana umaskini

**Na Jumanne Juma**

WANANCHI wameshauriwa kujiunga na Kampuni ya Jenga Afya Tokomeza (JATU), ili waweze kushiriki katika Soko la Hisa (DSE) na kuondokana na umaskini.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya JATU, Peter Isare, alisema hayo juzi katika Mkutano Mkuu wa tatu wa mwaka, unaolenga wanachama waweze kuingia kwenye mfumo wa hisa.

Isare alisema kampuni hiyo inatoa fursa kwa watu wanaoishi majumbani waweke hisa hizo hasa wanaowekeza katika kilimo cha kisasa na wanaotaka kumiliki viwanda.

"Ni muda wao sahihi kwa kuwa JATU inaenda kujikita kujenga viwanda vya kisasa, tunaposema uchumi wa kati na vya mkakati tayari tunalima parachichi, maharagwe, mahindi, mpunga, alizeti, viazilishe, vitunguu, ndizi na mboga," alisema Isare.

Pia, alisema JATU inatoa fursa kwa jamii kushiriki kupitia hisa watakazonunua hasa kwa vijana wanaotaka kuingia kwa ajili ya kuwekeza kwa kuwa kampuni hiyo inaingia kwenye soko la hisa.

Aidha, aliiomba serikali kutoa elimu ili vijana waweze kupata mazingira yatakayomwezesha kuingia kwenye kampuni za ndani ambazo zinaleta mabadiliko chanya katika jamii.

Naye mwenyekiti wa bodi wa kampuni hiyo, Dk. Zaipuna Yonah, aliwataka vijana wachukue nafasi zao kuwekeza na kuondokana na umaskini.

"Ninawataka vijana wajitokeze kuwekeza waondokane na fikra ya kusema wazee ndiyo wawekezaji, hivyo wajitokeze kwa kuwa wanaingia kimfumo wanapata fedha zao, ili kuleta maendeleo," alisema.

Mwanachama wa kampuni hiyo, Isabella Abraham, alisema, amewekeza kwenye kilimo cha mahindi eneo la Kiteto, mkoani Arusha, mpunga analima mkoani Morogoro na maharagwe mkoani Tanga.




Mkuu wa Kitengo cha Mazingira wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Modester Mushi (katikati), akiwa na wajumbe wa kamati za kushughulikia malalamiko (Grievances Readness Mechanism) katika utekelezaji wa mradi wa maji awamu ya pili wa Benki ya Dunia (WSSPII) wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yajipanga kuboresha huduma kimtandao

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya United for Africa Tanzania (UBA), imesema imejipanga kuboresha zaidi huduma za kimtandao, ili kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Kingsley Ulinfun, baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo juzi.

"Matarajio yangu makubwa kwa ajili ya wateja wa UBA Bank ni katika kutilia mkazo zaidi kwenye kuboresha huduma za kimtandao pamoja na bidhaa zenye kugusa maisha ya wateja wa benki yetu, ikiwa ni moja ya malengo yake ya muda mfupi," alisema Ulinfun.

"Tunataka kuboresha huduma kwa wateja wetu na kuongeza taratibu zetu za kuwahudumia pamoja na kuweka mfumo bora wa kibenki. Pia tunatarajia kuanza safari ya mabadiliko ya kidigitali ili kufanya huduma zetu ziwe za kirafiki zaidi."

Alisema kuwa benki ya UBA itaendelea kufanya kazi na wadau pamoja na washirika wake mbalimbali kama ambavyo imekuwa ikifanyika siku zote.

"Benki ya UBA Tanzania ni kampuni tanzu ya UBA Group ambayo inafanya kazi kwenye nchi 20 barani Afrika na imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo kwa kuunga mkono miradi mbalimbali ya serikali, kwa hiyo tutahakikisha kwamba tunaendeleza hili," alisema Ulinfun.

Mwenyekiti wa Bodi ya UBA, Tuvako Manongi, alisema kuwa wanaamini kuteuliwa kwa mkurugenzi huyo mpya kutaleta ufanisi zaidi wa huduma katika benki hiyo na ushindani imara.

"Tumepata mtu mwenye nguvu, ambaye ana shauku kubwa na hamasa kwenye masuala ya kibenki hasa kwenye nyakati hizi za ushindani mkubwa, tuna imani atatoa matokeo mazuri," alisema Manongi.

"Pia tumefurahi kusikia mipango yake ya kuboresha benki yetu ikiwamo kuleta mabadiliko chanya kwenye biashara na ukuaji wa uchumi wakati bara hili likipambana zaidi kwenye ukuaji wa teknolojia ya mtandao."

Mwisho.


**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU WAAJIRIWA KUWA NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) KABLA YA TAREHE 31 DISEMBA, 2020

***Dar es Salaam, 16 Novemba, 2020:***

Ikumbukwe kwamba mnamo tarehe **6 Agosti 2020,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilizindua mfumo wa uwasilishaji ritani za kodi kwa njia ya mtandao **(e-Filing)** ambapo, pamoja na ritani zingine, mfumo huu unajumuisha ritani ya zuio katika mapato ya waajiriwa, yaani, Pay As You Earn (PAYE).

Kutokana na mabadiliko hayo kuanzia sasa kila mwajiri atalazimika kuwasilisha ritani ya zuio katika mapato ya waajiriwa (PAYE) ikionesha namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) ya kila mwajiriwa na kodi husika iliyokatwa.

Kwa waajiriwa ambao TIN tayari wanazo, mwajiri ataziingiza katika ritani zake kuonesha kiasi cha kodi kilichokatwa kwa mwajiriwa husika na kuwasilishwa TRA.

Aidha, kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, na kwamba ama wana Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) au Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN), wanaelekezwa kuomba TIN hizo kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambao ni **www.tra.go.tz**). Kwa waajiriwa wasio na Kitambulisho cha Taifa watalazimika kutembelea Ofisi za TRA kupigwa picha na kuchukuliwa alama zavidole.

Hata hivyo, waajiri wanaelekezwa kuwa kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, waajiri wataingiza namba ya TIN ya mfano ambayo ni **999 999 999** wakati wa kuwasilisha ritani za kodi ya ajira kwa ajili ya kuwezesha kushughulikia mishahara yao.

Vile vile, tunapenda kutaarifu kwamba ukomo wa utaratibu huu kwa wasio na TIN ni hadi mnamo **tarehe 31 Desemba 2020.** Baada ya hapo hakutokuwa na muda wa nyongeza. Hivyo, tunawaomba na kuwasihi waajiri na waajiriwa wote wajitahidi kutekeleza wajibu wao katika muda uliowekwa hasa ikizingatiwa kuwa mlipakodi anapaswa kuwa na TIN ikiwa ni matakwa ya **Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019.**

Kwa maelezo zaidi; unaweza kutembelea Ofisi ya Mamlaka iliyo karibu nawe. Pia, unaweza kutembelea tovuti ya TRA **(www.tra.go.tz)** au kupiga simu bure kupitia **0800 750 075** au **0800 780 078,** na kutuma ujumbe wa WhatsApp (0744 23 33 33) au kutuandikia barua pepe kwa anwani pepe **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na;**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI TRA MAKAO MAKUU**

# KUPANDA SARUJI

## ■Ma-RC watoa maagizo

Na Waandishi Wetu

LICHA ya viongozi wa mikoa na wizara kuingilia kati sakata la kupanda kwa bei ya saruji nchini na kuwaonya wafanyabiashara wanaopandisha, bado hali haijatengemaa.

Mkoani Mbeya, Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, amemwandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, kumshauri aitishe mkutano wa kitaifa wa wadau wa saruji ili kujadili tatizo la kupanda kupita kiasi kwa bei ya bidhaa hiyo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Kiwanda cha Saruji cha Mbeya Cement na kushuhudia uzalishaji wa bidhaa hiyo ukiendelea kwa gharama ile ile na kuuzwa kwa bei elekezi, lakini mtaani ikiuzwa kwa bei ya juu.

Alisema kwenye barua hiyo alimshauri Katibu Mkuu huyo kuitisha kikao cha pamoja na kuweka utaratibu ambao utatumika kudhibiti mfumuko wa bei ya bidhaa hiyo muhimu.

Chalamila alisema kwa sasa bei ya saruji imepanda kupita kiasi na imegeuka kuwa kero kwa wananchi hali inayoweza kukwamisha maendeleo ya taifa.

"Tunatakiwa kuwa na kikao cha pamoja kati ya wadau wa usafirishaji na wazalishaji wa saruji ili tuwe na sauti moja, lengo langu ni kutaka Mtanzania asiumizwe mahali popote alipo kwa sababu ya watu wachache wanaotaka kujinufaisha," alisema Chalamila.

Aliusifu uongozi wa kiwanda cha Mbeya Cement kwa kuendelea kuzalisha bidhaa hiyo kwa wingi na kuiuza kwa bei ya kawaida, huku akiwalaumu wafanyabiashara ambao wanapandisha bei kwa makusudi mitaani.


Meneja mauzo wa kiwanda hicho, Godlisten Mende, alisema uongozi ulibaini uhaba wa bidhaa mtaani, lakini ukaamua kuendelea kuzalisha na kuuza bidhaa hiyo kwa bei ya zamani.

Alisema hawajawahi kusimamisha uzalishaji wa bidhaa hiyo, lakini hawaelewi chanzo cha uhaba mitaani uliosababisha kupanda kwa bei kupita kiasi hukuakidai kuwa wanaoathirika na kupanda kwa bei hiyo ni wananchi wa kawaida.

Alisema uongozi wa kiwanda hicho baada ya kubaini uhaba wa bidhaa hiyo mtaani uliwaandikia barua wasambazaji kuwaelekeza wasipandishe bei holela kwa lengo la kujinufaisha na kuwaumiza wananchi.

"Hatua inayohitajika kwa sasa ni kuongeza mawasiliano kati ya wasambazaji na wauzaji wa jumla, hii itatusaidia kupunguza tatizo wafanyabiashara kujipangia bei zao tofauti na zile zilizoelekezwa na serikali," alisema Mende.

Baadhi ya wadau wa usambazaji wa saruji waliiomba serikali iwasikilize wadau wa bidhaa hiyo kutokana na matatizo mengi yanayojitokeza kwenye mnyororo wa uuzaji ambayo yanasababisha gharama kuongezeka.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati (kushoto), akitoa maelekezo jana, kwa mmiliki wa kampuni ya Vimajo and Sons ambaye ni miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa wa saruji, Victor Chami (kulia), wakati wa ziara ya kukagua maduka ya wauzaji wakubwa na wadogo wa saruji ili kujionea hali halisi ya upatikanaji wake. **PICHA: VICENT TIGANYA**

Alisema wafanyabiashara wengi wanapandisha bei, ili kufidia matatizo yanayojitokeza kabla bidhaa hiyo haijaanza kuwafikia watumiaji wa mwisho.

Ukomo wa bei elekezi ya saruji kwa Mkoa wa Mbeya ni kati ya Sh. 17,000 na Sh. 18,000 kwa mfuko wa kilogramu 50, lakini kwa sasa wafanyabiashara wanauza mpaka Sh. 25,000.

**TABORA**

Mkoani Tabora Mkuu wa Mkoa, Dk. Philemon Sengati, amewaonya wafanyabiashara kutotumia soko huria na upungufu wa saruji kuwaumiza wananchi wanyonge kwa kuongeza bei ili kupata faida kubwa.

Akizungumza katika ziara ya kukagua maduka ya wauzaji wakubwa na wadogo wa bidhaa hiyo, na kujionea hali ya upatikanaji wake, alisema wafanyabiashara ni wadau muhimu wa kushirikiana na serikali kwenye shughuli za maendeleo ni vyema wakahakikisha inauzwa kwa bei nafuu ambayo haiwaumizi wananchi.

"Kwa nadharia ya soko huria bidhaa zinapopungua sokoni bei zinapanda...nawataka wafanyabiashara wa simenti wasitumie mazingira hayo ya uhaba kufidia kupata 'super profit' (faida kubwa) ambayo inawaumiza wananchi," alisisitiza.

Aliwaonya pia wafanyabiashara wa saruji wa maduka ya rejareja ambao wanauza kwa bei ya juu kinyume na elekezi kuacha mara moja na kwa kuwa serikali itawachukulia hatua watakaokaidi.

Alisema haiwezekani wanunue kwa kiwango Sh. 19,000 na kutaka kuuza kwa Sh. 23,000, nyongeza Sh. 4,000.

Dk. Sengati alisema kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na wauzaji wa jumla ambao wanapata faida ya Sh. 200 kwa mfuko na gharama za kusafirisha mzigo kutoka viwandani ni kubwa.

"Tumebaini wafanyabiashara wa rejareja wanauza saruji kwa Sh. 23,000 hadi 30,000 wakati bidhaa hizo amechukulia hapa hapa Tabora na hana gharama kubwa za kusafirisha mizigo...kitendo hicho ni kutaka kutengeneza fedha nyingi kwa kuwaumiza wanyonge... hakikubaliki, serikali haiwezi kuvulimia, tutawachukulia hatua," alisema.

Naye mmiliki wa Kampuni ya Vimajo and Sons, ambaye ni miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa wa saruji mkoani humo, Victor Chami, alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa yeye anauza mfuko wa kilo 50 kwa Sh. 19,000 baada ya kuwapo kwa uhaba wa saruji kutoka Sh. 18,500 kabla ya tatizo.

Alisema saruji inapatikana kwa shida na wakati mwingine wanalazimika kununua kwa wafanyabiashara wenzao ambao wana akiba.

Mfanyabiashara huyo aliongeza kuwa hivi sasa wameamua kununua saruji aina ya Camel baada ya waliyokuwa wakinunua kwa wingi mkoani Tabora ya Dangote, kutopatikana.

Alisema wananunua saruji hiyo kwa Sh. 13,340 kiwandani Dar es Salaam na gharama za usafiri ni Sh. 5,000, vibarua wa kushusha wanawalipa Sh. 100 na zinazobaki ndio faida yao.

Chami alisema kutoka na uhitaji mkubwa wa saruji nchini kwa sababu ya miradi mikubwa inayojengwa na serikali na mahitaji ya wananchi ni vyema serikali ikawabana wenye viwanda ili waongeze uzalishaji.

Alisema serikali itakapokamilisha miradi yake, wazalishaji waruhusiwe kupeleka nje ya Tanzania.

Alimweleza Mkuu huyo wa Mkoa kuwa amesikia kilio cha wananchi, atauza saruji kwa bei ya awali ya Sh. 18,500 kama ilivyokuwa kabla ya kuadimika.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wenzake kuangalia uwezekano nao kushusha ili wananchi wasiumie.

**DAR ES SALAAM**

Jijini Dar es Salaam, licha ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kufanya ziara kwenye viwanda na maduka ya jumla na rejareja na kuelekeza iuzwe kwa Sh. 15,000, bado bidhaa hiyo inauzwa kati ya Sh. 15,500 hadi 16,500.

Katika eneo la Kiluvya wafanyabiashara wa rejareja walisema faida yao kwa kila mfuko ni Sh. 500 hadi 1,000 na wananunua mkoani Pwani kwa kuwa inayozalishwa na kiwanda cha Twiga haipatikani.

"Tunanunua bei ya juu, tunaomba serikali ishughulike na wauzaji wa jumla pamoja na viwanda kuliko kutubana sisi ambao hata kuipata ni shida na tunaipata kwa bei ya juu," alilalamika Michael Tarimo, muuzaji wa dula la rejareja.

Katika eneo la Salasala mfuko mmoja unauzwa Sh. 15,500.

**KAULI YA SERIKALI**

Akijibu sababu ya kupanda kwa saruji, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovick Nduhiye, alisema kuadimika kwa bidhaa kutokana na viwanda vingi kutumia kipindi cha uchaguzi kutengeneza viwanda vyao.

"Mara nyingi wazalishaji wa saruji wamezoea kwamba inapofika katika uchaguzi miradi mingi ya serikali husimama na hivyo kutokuwa na uhitaji mwingi wa bidhaa hiyo, lakini tofauti na miaka mingine, mwaka huu ilikuwa tofauti, miradi yote iliendelea kama kawaida na kuendelea kuhitaji saruji nyingi," alisema Nduhiye akihojiwa na TBC.

"Ndiyo maana kwa namna nyingine saruji ilipanda kwa kiwango kikubwa."

Alisema kutokana na viwanda vingi kusitisha uzalishaji kwa ajili ya matengenezo, Oktoba ilikuwa na upungufu wa tani 300,000 za saruji hiyo.

"Julai mwaka huu kulikuwa na jumla ya tani zaidi ya 300,000, Agosti zaidi ya tani 400,000, Septemba zaidi ya tani 400,000, lakini Oktoba iliingia tani zaidi ya 100,000 tu na kufanya upungufu wa tani 300,000.

Alisema, baada ya kuadimika kwa saruji hiyo, serikali ilichukua hatua ya kuchunguza kama ilikuwa na mchezo kwa wazalishaji.

Pia alisema wanatarajia katikati ya mwezi huu hali ya upatikanaji wa bidhaa hiyo itarudi katika hali ya kawaida.

"Tumejipanga kwamba hali ya upatikanaji wa saruji itarudi katika hali ya kawaida ikiwamo kuwashughulikia wale ambao watabainika kuhujumu," alisema.

**■Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR), Nebart Msokwa (MBEYA) na Tiganya Vincent (TABORA)**

# Wajawazito wasiohudhuria kliniki kupewa adhabu

**Na Yasmine Protace,**
DODOMA

SERIKALI ya Kijiji cha Mundemu, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, imeweka utaratibu ambao mjamzito asipohudhuria kliniki, anapewa adhabu ya kufanya usafi na mumewe.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya kubaini baadhi ya wajawazito kushindwa kuhudhuria kliniki pasipo sababu, na hali hiyo imekuwa ikichangia kupata matatizo wanapojifungua.

Hayo yalisemwa na Stephen Daudi, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Tarafa ya Mundemu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu faida zilizopatikana kupitia mradi wa Tutimize Ahadi, ulioratibiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Restless Development.

"Mradi wa Tutimize Ahadi, ulipoingia kijijini umeleta mabadiliko makubwa kwa jamii, awali matukio ya ukatili, afya ya uzazi, wananchi wa hiki kijiji walikuwa hawajitambui, hivyo elimu ilipoanza kutolewa kupitia mradi huo jamii iliweza kujitambua," alisema.

Aliongeza kuwa katika kujitambua kwao, wanaofanyiwa ukatili, wameanza kutoa taarifa na wahusika wanachukuliwa hatua.

Kadhalika, alisema afya ya uzazi jamii imejitambua kwa sasa, ambapo vijana wanafika vituo vya afya na kupatiwa elimu ya uzazi wa mpango.

Alisema serikali ya kijiji ikiwahamasisha wajawazito kushiriki vituo vya afya na wenza wao, ili waweze kuhudhuria kliniki walipotakiwa kwenda.

Alisema wanafuatilia kuona mama mjamzito na mwenza wake kama wanaenda kliniki, na wakibaini hawajaenda wanawakamata na kuwapeleka kufanya usafi katika kituo cha afya. "Wapo baadhi ya wajawazito na wenzao wao, ambao wanakaidi kuhudhuria kliniki, nasi tukibaini hilo, tunawafuatilia na kuwakamata na kuwapa eneo katika kituo cha afya ili wafanye usafi siku nzima," alisema Mundemu.

Aliongeza kuwa kuwafanyisha usafi ni moja ya sababu ambayo wanaitumia, ambapo imezaa matunda makubwa ya mahudhurio ya kliniki na wanaokwepa kwenda wanawakamata na kuwafanyisha usafi siku nzima.

Aliongeza kuwa mahudhurio ya kliniki pia yanamsaidia hata mjamzito wakati wa kujifungua asipate tatizo lolote hivyo kujifungua mtoto salama.



Mmoja wa madaktari kutoka kituo kinachotoa huduma za kisukari St. Laurent, akimpima mwananchi aliyejitokeza kwenda kupima afya katika maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yajipanga kuhudumia ongezeko la wawekezaji

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamazi wa Mazingira (NEMC) limesema kuna uwezekano mkubwa wa miradi ya biashara na uwekezaji kuongezeka mara mbili katika kipindi cha pili cha uongozi wa Rais John Magufuli, hivyo linajipanga kuhudumia ongezeko hilo.

Akizungumzia mkakati wa baraza wa uwezeshaji wa wenye miradi ya biashara na uwekezaji kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema NEMC ni chombo wezeshi katika kuhakikisha biashara na uwekezaji nchini vinafanyika kwa urahisi na kwamba baraza limefanya maboresho ya kiutendaji kukidhi mahitaji ya siku za usoni.

Tunaimani kuwa katika awamu hii ya pili ya uongozi Rais John Magufuli idadi ya miradi ya biashara na uwekezaji itaongezeka mara mbili. Ili kukabiliana vizuri na hali hiyo, tumeboresha mifumo na mazingira ya utendaji kazi wa ofisi yetu, alisema Dk. Gwamaka.

Alisema Tanzania ni nchi nyenye mvuto kwa wawekezaji wa duniani na wa kikanda, ina misingi imara ya demokrasia ni salama; Watanzania ni wakarimu na serikali ina uhusiano mzuri sana na sekta binafsi.

Alifafanua kuwa serikali pia ni makini juu ya utumiaji wa fursa mbalimbali na ukuzaji wa biashara kikanda na ujenzi wa miundombinu hasa barabara, reli, umeme na TEHAMA.

"Hoja zote hizi katika umoja wake zinatoa msingi wa kuona ongezeko maradufu la miradi ya biashara na uwekezaji katika miaka mitano ijayo ya serikali ya Rais Magufuli," alisema.

Alisema baraza limeendelea kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kuondoa ukilitimba na urasimu, tabia ambazo zimekuwa zikipunguza ufanisi katika utendaji kazi.

Tumeondoa urasimu na vitendo vya rushwa kwa watendaji wetu, jambo ambalo lilikuwa likizorotesha utendaji kazi wa baraza na pia kupunguza kasi ya uwekezaji nchini kutokana na kuchelewesha vibali," alisema Dk. Gwamaka.

Amesema NEMC imejenga utamaduni wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wawekezaji juu ya Sheria ya Mazingira ya 2004 na kanuni juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira ili kuwajengea uwezo na uelewa wa kile wanachotaka kukifanya kabla ya kusajili miradi yao.

Alisema ujenzi wa uchumi wa viwanda unategemea ushirikiano wa taasisi za umma katika kutoa huduma wezeshi kwa wawekezaji na wafanyabiashara jambo litakalochochea ukuaji wa pato la taifa.

# Watakiwa kupima kudhibiti kisukari

**Na Christina Mwakangale**

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kupima afya zao mara kwa mara ili kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo ugonjwa wa kisukari ambao hadi sasa umeathiri zaidi ya watu milioni 1.5.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mawasiliano ya Abel & Fernandes, Fatma Fernandes wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani yaliyofanyika katika kituo kinachotoa huduma za kisukari cha St. Laurent.

Maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila Novemba 14, yalienda sambamba na utoaji wa huduma za upimaji na ushauri wa kitabibu bure.

Katika maadhimisho ya mwaka huu yalidhaminiwa na Kampuni ya Abel & Fernandes Communications pamoja na Quincewood Consulting kupitia miradi yake ya uwajibikaji kwa jamii.

Aidha, katika maadhimisho hayo, kampuni hizo zimeungana na Kituo cha Kisukari St. Laurent katika kuisaidia serikali katika mapambano dhidi ya kisukari kwa kujenga uelewa kuhusu ugonjwa huo, ambao kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya hadi sasa umeathiri zaidi ya watu milioni 1.5 nchini.

Mkurugenzi wa Kituo cha Kisukari, St Laurent, Dk. Mary Maige, alisema kauli mbiu ya maadhimisho ya Kisukari duniani kwa mwaka huu ni "Uuguzi na Kisukari".

Alisema mwaka 2012 walifanya utafiti nchi nzima na kubaini kati ya watu 10, watu watano wana tatizo la kuchakata sukari mwilini, hivyo kubaini kuwa asilimia 20 ya Watanzania wana matatizo ya kuchakata kisukari.

"Kwa hiyo hili tatizo linazidi kuongeza, na kadiri siku zinavyozidi kusonga mbele tatizo linaendelea kuongezeka na tunatakiwa kuongeza juhudi zaidi ili kudhibiti tatizo hili ambalo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mtindo wetu wa maisha," alisema.

Naye Katibu Mwenezi wa Chama cha Wauguzi Tanzania, Johari Yusufu, alisema kampeni hiyo ya mwaka huu inalenga kuwapa motisha wauguzi kutekeleza majukumu yao kwa uweledi ili kuwapatia huduma bora, stahiki na zenye staha wagonjwa wa kisukari nchini.

Alisema wauguzi wanahesabika kuwa nusu ya wafanyakazi wote wa sekta ya afya nchini. Ni kada mojawapo inayoweza kuwapatia huduma bora watu wanaoishi na magonjwa mbalimbali. Watu wanaoishi na kisukari huhitaji zaidi msaada wa wauguzi katika kutibu tatizo hilo.

"Kwa hiyo tunawashauri wananchi wawe wanakwenda hospitali kucheki afya zao mara kwa mara," alisema.

Meneja uhusiano wa Kampuni ya Abel & Fernandes Communications, Abbas Jabir, alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kwa pamoja wanaungana na wauguzi kuzuia na kutoa muongozo kuhusu Kisukari.

"Pia tunatoa huduma kwa mamia ya jamii kwa malengo ya kuwapatia taarifa muhimu kuhusu ugonjwa wa kisukari na namna ya kukabiliana nao.

# Walalamikia kupaa kwa bei ya limao

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAHITAJI makubwa ya malimao na ndimu katika masoko ya Kenya ambayo yanatumiwa kama tiba asili dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid-19) yamesababisha kupanda bei bidhaa hiyo.

Bei imepanda kutoka Sh. 500 hadi 2,000 kwa fungu la malimao katika masoko ya mjini Morogoro.

Baadhi ya wananchi katika Mkoa wa Morogoro wamewalalamikia wafanyabiashara hao katika masoko ya manispaa kwa kupandisha kwa kasi bei hiyo ya malimao, huku baadhi yao wakishindwa kuitumia bidhaa hiyo.

Ummy Peter, mkazi wa Kihonda Maghorofani Manispaa ya Morogoro, alisema kwa sasa bei ya limao haishikiki katika masoko ya Sabasaba na Mawenzi kutokana na limao moja kuuzwa kati ya Sh. 400 kwa limao dogo na shilingi 700 kwa limao kubwa tofauti na bei ya kawaida ilikuwa ikiuzwa Sh. 100 wakati wa kuwapo kwa tishio la maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 miezi michache iliyopita.

"Kipindi cha tishio la corona malimao yalikuwa mengi, katika soko la Mawenzi tulikuwa tukiuziwa kati ya shilingi 50 mpaka 100 kwa limao, tena kubwa sana na unabembelezwa na wafanyabiashara, lakini hivi sasa limao dogo ni shilingi 400 na kubwa 700 tena ni dogo na halina maji ya kutosha na ukitaka fungu wanauza shilingi 1,500 mpaka 2,000," alisema Ummy.

Naye Rehema Msuya, mkazi wa Mazimbu, alisema kutokana na kupanda kwa bei ya malimao katika masoko ya Manispaa ya Morogoro, analazimika kununua malimao yaliyosindikwa kwenye mifuko ya plastiki kwa bei ya shilingi 100 mpaka 200 kwenye maduka ya kawaida.

"Kwa kweli hivi sasa limao halishikiki huko sokoni bei ni kubwa sana, sasa sijui msimu umekwisha au mahitaji ya malimao yamekuwa makubwa, maana kipindi kile cha corona malimao tulikuwa tunanunua kwa bei ya kutupa sana," alisema Rehema. Baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa hiyo katika soko la Mawenzi, walieleza kuwa kupanda kwa bei hiyo ya malimao inatokana na wafanyabiashara wakubwa kufika sokoni hapo na kununua kwa bei ya jumla kutoka kwa wakulima na kusafirisha bidhaa hizo kuelekea Kenya kutokana na kuwapo kuwapo kwa mahitaji makubwa.

Shomari Mwinyi anayefanya biashara ya kuuza malimao soko la Mawenzi, alisema analazimika kuyafuata malimao hayo kwa wakulima mashambani katika vijiji vya Matombo, Kinole na Mgeta na kwenda kuuza katika soko la Mawenzi kutokana na bidhaa hiyo kuwa adimu.

"Malimao hivi sasa yamekuwa adimu sana...ninachokueleza kuna wafanyabiashara wakubwa wanatoka mikoa mbalimbali wanaenda huko vijijini kwa wakulima wananunua malimao yakiwa bado madogo kwa bei wanayotaka wakulima, limao moja linauzwa mpaka mia tano nasikia, wanasafirisha wanapeleka Kenya yanahitajika sana, kwa hiyo ndio maana bei imepanda ya malimao," alisema Shomari. Naye Tatu Shukuru mfanyabiashara wa malimao katika soko la Manzese, alisema bei ya malimao imekuwa juu tofauti na kipindi cha tishio la ugonjwa wa corona Machi mwaka huu, ambapo limao moja lilikuwa likiuzwa kwa shilingi hamsini mpaka mia moja huku fungu lenye malimao kumi makubwa likiuzwa kwa bei ya shilingi 500.

Alisema kwa sasa malimao hayo yamekuwa yakiuzwa kati ya shilingi 300 mpaka 500, huku f ungu la limao likiuzwa kati ya shilingi 1,000 mpaka 2,000 kutokana na wakulima kuwapandishia bei kwa sababu bidhaa hiyo msimu wa mavuno umeanza kuisha pamoja kuwapo kwa mahitaji katika masoko mengine nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (kushoto), akimkabidhi zawadi ya simu mteja wa muda mrefu wa Vodacom Tanzania Plc, Saleh Semjaila, wakati wa uzinduzi wa duka la kwanza la kampuni hiyo, wilayani humo, mkoani Pwani juzi. Wapili kushoto ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mwanana Msumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yahimizwa matumizi ya vyoo

**Na Timothy Itembe,** TARIME

JAMII imetakiwa kuondokana na tabia ya kujisaidia vichakani kwani kufanya hivyo ni moja ya njia ya kuchochea magonjwa ya mlipuko.

Mratibu wa Uelimishaji Afya na Ofisa Afya wa Halmashauri ya Mji wa Tarime mkoani Mara, Aggrey Hyera, alisema hayo katika mahojiano na gazeti hili juu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko.Hyera alisema ili kuondokana na magonjwa ya mlipuko, kuna haja jamii kuondokana na tabia ya kujisaidia vichakani, badala yake wajenge tabia ya kujisaidia chooni na choo hicho kiwe bora.

Aliongeza kuwa hataraji kuona binadamu ambaye anaishi karne ya 21 hana choo badala yake watu wake wanaenda kujisaidia porini, jambo ambao ni hatari kwa afya ikiwamo kueneza maambukizi ya magonjwa ya mlipuko. "Magonjwa ya mlipuko kama vile kuhara damu, magonjwa ya matumbo yote hayo yanatokana na binadamu kula kinyesi...kwa maana hiyo lazima sasa jamii iondokane na tabia ya kujisaidia porini badala yake ijenge tabia ya kwenda kujisaidia chooni na kufanya hivyo ni moja ya maendeleo," alisema Hyera.

# DC Gondwe asisitiza elimu kwa wajasiriamali

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam, Godwin Gondwe, amezitaka taasisi za fedha kuongeza nguvu zaidi katika kuwaelimisha wajasiriamali kufahamu namna bora ya usimamizi wa fedha ili waweze kukua zaidi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya benki ya NBC ijulikanayo kama 'NBC Kua Nasi' yenye lengo la kuwawezesha wajasiriamali kutunza fedha zao kwa usalama bila gharama za uendeshaji.

DC Gondwe alisema hatua hiyo ni muhimu katika utekelezaji wa mipango ya serikali ikiwamo kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma nafuu za kibenki.

"Akaunti hii ni fursa kwa vijana, kinamama na wajasiriamali wote, kwanza unaweka fedha zako na hakuna malipo ya mwezi na pili akaunti hii inaambatana na kutoa elimu ya kibenki, hii ni sehemu ambayo tulikuwa hatujaitilia mkazo hasa kwa wajasiriamali wadogo," alisema Gondwe.

"Mwaka jana tumetoa zaidi ya Sh. bilioni 2.6 za mikopo kwa wajasiriamali wadogo, hii huduma imekuja wakati muafaka ili waweze kufahamu namna bora zaidi ya kutunza fedha," alisema.

Mkurugenzi wa Fedha wa NBC, Waziri Barnabas, alisema akaunti hiyo inawawezesha wafanyabiashara wadogo kukuza biashara zao kwa kuweka pesa kwa urahisi na unafuu kwani huduma hiyo inapatikana mahali popote kwa njia ya simu (NBC Kiganjani).

Alisema kupitia 'NBC Kua Nasi' wafanyabiashara wadogo kama mamalishe, madereva bodaboda, wasindikaji pamoja na wasusi wataweza kuhifadhi pesa zao kwa urahisi zaidi na kuacha kukaa na pesa taslimu njia ambayo si salama.

"Makundi haya yanaajiri watu wengi sana na ufikaji wa huduma za kifedha kwao umekuwa mgumu na mara nyingi wanakaa na fedha mkononi, hivyo akaunti hii ni sehemu ya mpango wa benki yetu katika kuhakikisha tunawafikia watu wengi zaidi kuwapatia huduma za kifedha zinazoendana na shughuli zao za kiuchumi," alisema Barnabas.

Aidha, mteja ataweza kupata riba ya hadi asilimia 2 atakapoweka fedha kwenye akaunti hiyo ndani ya mwaka.

Mmoja wa wafanyabiashara, Dativa Ngowi, alisema huduma hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa kupunguza gharama za uendeshaji za kila mwezi pamoja na makato ya kutoa pesa.

Nipashe Spotika




MAKINDA 10 WAKUTAZAMWA LIGI YA MABINGWA ULAYA 2020-21 UK. 12&13




Ronaldo

# WACHEZAJI WATANO WENYE MABAO MENGI YA 'FREE-KICK'

**LONDON, England**

NI goli gani tamu kwenye soka? Mchezaji kumpiga chenga mlinzi na kufunga? Mkwaju wa penalti? Kufunga kwa kumpiga kanzu golikipa? Bao la adhabu ndogo "free-kick"?

Mashabiki wa soka wanajua kwamba, kufunga bao kwa shuti la free-kick ni sanaa. Kumekuwa na wachezaji wengi wenye uwezo huo kwa kipindi cha nyuma.

Nyota kama Juninho, Roberto Carlos, Ronaldinho na David Beckham ni miongoni mwa wachache waliokuwa na kipaji hicho.

Kuwa na mchezaji kwenye timu mwenye uwezo mkubwa wa kufunga kwa mashuti ya adhabu ndogo ni faida kwa timu, kwani ana uwezo wa kuipa ushindi wakati wowote.

Katika kizazi cha sasa kuna wachezaji wenye kipaji hicho, ambao wanaweza kufunga mabao matamu kwa mashuti ya adhabu ndogo.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji watano wenye mabao mengi yanayotokana na mashuti ya adhabu ndogo, unawajua? Hawa hapa....

**#5. Aleksandar Kolarov - Mabao 22**

Aleksandar Kolarov ni mmoja wa mabeki wa pembeni wenye uwezo mkubwa wa kufunga kwa adhabu ndogo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefunga asilimia 35 ya mabao yake kwa free-kick, kitu ambacho ni cha kuvutia, hasa kwa mlinzi.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester City na AS Roma, mara kwa mara amekuwa akitwa Roberto Carlos wa Serbia, kwa sababu ya nguvu yake yake ya kupiga mashuti kama iliyokuwa kwa gwiji huyo wa Brazil.

Kinachompa sifa zaidi ni uwezo wake wa kufumua mashuti kwa umbali mrefu katika sehemu yoyote.

Moja ya mabao yake yanayokumbukwa zaidi ni lile alilofunga wakati Serbia ikicheza na Costa Rica kwenye fainali za Kombe la Dunia mwaka 2018 na lile aliloifungia AS Roma kwenye mchezo wa maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Athletic Bilbao mwaka jana.

**#4. Hakan Calhanoglu - Mabao 26**

Kama wewe ni mtu unayefuatilia soka la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, utakuwa unamjua vizuri Hakan Calhanoglu hasa kutokana na uwezo wake wa kupiga mashuti. Anafunga kutoka upande wowote mpira utakapotengwa.

Asilimia 38 ya mabao yake kwenye klabu hiyo ya Ujerumani (akiwa pia ameichezea timu ya daraja la chini ya Karlsruher SC) yametokana na mashuti ya free kick!

Pia nani anayeweza kusahau msimu wa 2014-15 wakati alipofunga mabao tisa ya free-kick kwa Bayer Leverkusen! Ndio, kwa msimu mmoja!

Bahati mbaya, Calhanoglu ile nguvu yake ya kufunga mabao hayo imepungua tangu alivyohamia AC Milan mwaka 2017; kwani amefunga matatu tu.

**#3. Miralem Pjanic - Mabao 26**

Licha ya kufunga mabao mengi ya free kick kama Calhanoglu, nyota huyo wa kimataifa wa Bosnia, Miralem Pjanic, anatajwa kama mmoja wa wachezaji wenye rekodi nzuri zaidi.

Amecheza pamoja na Cristiano Ronaldo na Paolo Dybala pale Juventus, lakini Pjanic ana rekodi nzuri zaidi ya kufunga free-kick kwa 'Bianconeri' hao kuliko wachezaji hao wawili.

Pjanic, ambaye kwa sasa amesajiliwa kule Barcelona, pengine anaweza kuwa msaidizi wa Lionel Messi, ingawa atatakiwa kuonyesha uwezo mkubwa zaidi ili aweze kuaminiwa na 'Blaugrana' hao.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao 22 ya free-kick katika klabu hiyo, huku mengine manne akifunga kwa timu yake ya taifa. Cha kufurahisha ni kwamba asilimia 68 ya mabao yake ya free-kick yamekuja katika miaka mitano iliyopita, hivyo kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani katika nafasi hiyo.

**#2. Lionel Messi - Mabao 53**

Lionel Messi amefunga mabao 21 ya free-kick kwa klabu na timu ya taifa kwa misimu mitatu tu iliyopita.

Messi hakuwa mpigaji wa free-kick kiasili. Lakini hilo amekuja kulifanya baadaye na amekuwa mzuri zaidi kwa mipira hiyo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa bora zaidi kwa kufunga free-kick kwa sasa, si tu kwa kufunga, hata kwa pasi za mwisho.

Unakumbuka lile bao la umbali wa yadi 35 alilofunga dhidi ya Liverpool mwaka jana? Au lile dhidi ya Marekani mwaka 2016, au lile dhidi ya Real Madrid mwaka 2012? Tunaweza kuyaorodhesha mengi sana!

Kwa sasa ana mabao 53 ya free-kick, huku 47 akifunga pale Barcelona na mengine akifunga akiwa na jezi ya timu ya Taifa ya Argentina.

**#1. Cristiano Ronaldo - Mabao 57**

Cristiano Ronaldo anabaki kuwa bora zaidi kwa mipira ya free-kick, lakini nguvu yake inaonekana kushuka katika miaka ya hivi karibuni.

Uwezo wa Ronaldo kufunga kwa mashuti ya adhabu ndogo ni mkubwa zaidi na pengine kutokana na umri kwenda, uwezo wake kwa sasa unashuka, lakini bado anasimama kama kinara.


Amefunga mabao mengi sana ya free-kick kuanzia kule Manchester United, Real Madrid na sasa Juventus.

Pia kwa timu yake ya Taifa ya Ureno ndiye kinara asiyepingika, kwani hadi sasa anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwa kikosi hicho.

Alifikisha mabao 100 aliyoifungia timu yake ya taifa yakiwa mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa timu ya taifa kwa Bara la Ulaya.

## ISIKUPITE

BEKI wa Hispania, Sergio Ramos ameweka rekodi ya kuwa mwanasoka wa kwanza Ulaya kuichezea timu ya taifa mechi nyingi zaidi, baada ya kumpiku nguli wa Italia, Gianluigi Buffon. Jumamosi Ramos aliichezea Hispania mechi ya 177 wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Uswisi, ikiwa ni baada ya Jumatano kuifikia rekodi ya Buffon ya mechi 176 wakitoka sare kama hiyo dhidi ya Uholanzi. Kwa maana hiyo Ramos amebakiza mechi nane tu kuifikia rekodi inayoshikiliwa na kiungo wa zamani wa Misri, Ahmed Hassan.



## Extra Time

# MAKINDA 10 WAKUTAZAMWA LIGI YA MABINGWA ULAYA 2020-21



Haaland

**LONDON, England**

LIGI ya Mabingwa Ulaya ni michuano mikubwa inayoshirikisha timu 32 bora kwenye bara hilo. Kwa miaka mingi, wachezaji wengi wameweka alama yao kwenye ligi hiyo.

Wayne Rooney aliweka alama ya kuanza kucheza michuano hiyo kwa kufunga hat-trick miaka 15 iliyopita.

Hivi karibuni, kinda kutoka Norway, Erling Braut Haaland alijitambulisha yeye mwenyewe kwa kufunga hat-trick kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na kuwa mchezaji wa tisa katika historia ya mashindano hayo kufanya hivyo.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10-bora vijana ambao wanaweza kuleta mchango mkubwa kwenye mashindano hayo msimu huu wa 2020-21, hawa hapa...

**#10. Ryan Gravenberch (Ajax)**

Ryan Gravenberch ni mchezaji aliyetokea kwenye akademi ya Ajax. Kiungo huyu wa kati, ambaye anaweza kucheza kama kiungo mkabaji, aliweka historia ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi pale Ajax wakati alipoanza kucheza kwenye msimu wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, msimu wa 2019-20.

Alianza kucheza akiwa na umri wa miaka 16 na Gravenberch amecheza mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. Bado hajatoa mchango wa bao, lakini ni mmoja wa wachezaji wa kuchungwa sana kwenye mashindano haya.

Mchezaji wa zamani wa Uholanzi, Ronald de Boer amebainisha kwamba, Gravenberch ni mmoja wa wachezaji wakali wenye kipaji kikubwa zaidi kuliko Matthijs de Ligt.

**#9. Giovanni Reyna (Borussia Dortmund)**

Giovanni Reyna ni mmoja wa wachezaji wanaotabiriwa makubwa zaidi katika soka la Marekani. Baada ya kuwasili hapo akitokea Borussia Dortmund kipindi cha majira ya joto kilichopita, Reyna mara kwa mara amekuwa akilinganishwa na Christian Pulisic kwa staili yake ya uchezaji.

Reyna tayari amefunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho saba katika mechi 29 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo ya Bundesliga. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji bado hajafunga katika mechi tano za mashindano ya Ligi ya Maingwa Ulaya, lakini tayari ametoa pasi ya mwisho moja.

Mkurugenzi wa Dortmund, Carsten Cramer, anaamini klabu ilishinda kamari kwa kumsajili Reyna.

**#8. Eduardo Camavinga (Rennes)**

Eduardo Camavinga, katika msimu wake wa kwanza, mzaliwa huyo wa Ureno mwenye uraia wa Ufaransa, alikuwa nguzo ya kiungo kwa klabu hiyo ya Ligue 1, ambayo ilimaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo na kufanikiwa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika umri wake wa miaka 17, nyota huyo ameonyesha uwezo wa kuvutia zaidi dimbani. Hata hivyo, kufunga ni sehemu ambayo anaweza kuimarika zaidi - Camavinga amefunga mara mbili katika mechi 52 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo.

Zaidi ni kwamba, kinda huyo aliweka historia ya kuwa mchezaji wa pili mdogo zaidi wa Ufaransa kufunga bao, na anaweza kujiongeza zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#7. Eric Garcia (Manchester City)**

Eric Garcia aliripotiwa kuwa ni mmoja wa nyota waliokuwa wanawaniwa zaidi na Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita kabla ya Manchester City kukaza uzi na kumbakisha.

Kulikuwa na sababu nzuri kwa nini Man City waliamua kumbakisha Garcia. Chini ya mwalimu Pep Guardiola, Garcia ameonyesha namna gani alivyopevuka kwa kuwasaidia John Stones na Nicolas Otamendi, huku akitengeneza upatina mzuri na Aymeric Laporte kwenye safu ya ulinzi.

Na wakati mchezaji huyo akikubali kubakia na klabu hiyo angalau kwa msimu mwingine mmoja, anaweza kuwa suluhisho la timu hiyo katika safu ya ulinzi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

**#6. Curtis Jones (Liverpool)**

Zinaweza kuwa siku nzuri kwa kinda, Curtis Jones kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na tayari ameshaonyesha umuhimu wake kwa kikosi cha Liverpool.

Msimu uliopita, kiungo huyo wa kati alikuwa mchezaji wa pili mwenye umri mdogo zaidi kwa kikosi cha Liverpool kufunga kwenye Ligi Kuu ya England, pia akifunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo.

Jones, ambaye ameimarika haraka katika kikosi cha Jurgen Klopp alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Atalanta msimu huu.

Kinda huyo anaonekana kuwa na muda mwingi zaidi wa kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu chini ya Klopp.

**#5. Joshua Zirkzee (Bayern Munich)**

Joshua Zirkzee alianza vizuri sana kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wakati alipoingia akitokea benchi na kufunga dhidi ya Freiburg na Wolfsburg. Mabao yake mawili ya kwanza yalimfanya kuwa mchezaji wa tatu mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Bayern Munich.

Raia huyu wa Uholanzi anaonekana kuwa ndiye mrithi sahihi wa Robert Lewandowski ambaye alifunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Ingawa Zirkzee hajafunga bao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, hilo linaweza kubadilika haraka, na anaonyesha ni mchezaji ambaye anaweza kubadilisha mambo haraka.

**#4. Mason Greenwood (Manchester United)**

Mason Greenwood ndio kwanza amefikisha umri wa miaka 19, lakini tayari amecheza mechi zaidi ya 61 kwa klabu yake na kufunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho sita. Kiukweli amekuwa mchezaji mwenye mchango mkubwa kwa klabu yake na amekuwa akifananishwa na gwiji, George Best.

Mmoja wa wahitimu bora wa akademi ya Manchester United katika miaka ya hivi karibuni. Greenwood alijitambulisha yeye mwenyewe kwenye Ligi Kuu ya England msimu uliopita, akifunga mabao 10, kitu kilichomfanya kuwa kinda wa kwanza katika misimu saba kufanya hivyo.

Msimu huu, Greenwood alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini yanaweza kuwa yanakuja mengi zaidi kwenye michuano hiyo kama ataendelea kuimarika.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer tayari anafikiria mengi kwa Greenwood, ambaye anaweza kuwa Muingeneza mwingine atakayekuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#3. Rodrygo (Real Madrid)**

Tofauti na wachezaji wengine kwenye orodha hii, kinda wa Real Madrid, Rodrygo tayari ameshaweka alama yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu uliopita, nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, alifunga hat-trick dhidi ya Galatasaray na kuwa mchezaji wa pili mwenye umri mdogo zaidi kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufanya hivyo.

Rodrygo ambaye ni nyota wa zamani wa Santos mara kwa mara amekuwa akilinganishwa na Robinho na Neymar. Amekuwa akiaminiwa na kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, kocha pekee kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kushinda taji hilo mara tatu mfululizo.

**#2. Ansu Fati (Barcelona)**

Ansu Fati msimu uliopita aliweka historia ya kuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mdogo zaidi kufunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati alipofunga dhidi ya Inter Milan.

Fati tayari ameonyesha kuimarika kwake chini ya kocha mpya wa Barcelona, Ronald Koeman msimu huu. Amefunga mabao manne kwenye La Liga - moja akifunga kwenye mchezo wa El Clasico wakati wakifungwa na Real Madrid na lingine kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akiwa na pasi za mwisho tatu.

Bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji bora waliohitimu kutoka akademi ya Barcelona, La Masia hivi karibuni tangu Lionel Messi, angeweza kufanya makubwa Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini amekubwa na majeraha yatakayomweka nje kwa muda mrefu.

**#1. Erling Braut Haaland (Borussia Dortmund)**

Erling Braut Haaland bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji vijana wanaovuma kwa sasa katika sayari hii. Ameichukua Ligi ya Mabingwa Ulaya kama bata kwenye maji.

Baada ya kufunga mara tisa kwa RB Salzburg kwenye mwanzo wake wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ikiwamo hat-trick katika mchezo wake wa kwanza, kinda huyo wa kimataifa wa Norway alipata nafasi ya kujiunga na Borussia Dortmund kipindi cha majira ya baridi, ambako ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

Mshambuliaji huyo wa kati mwenye umri wa miaka 20, tayari amefunga mabao manne kwenye mashindano hayo msimu huu.

Nyota wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Jermaine Jonas, amemwelezea Haaland kama ni mmoja wa washambuliaji waliokamilika duniani.

Anatajwa kuwa ndiye nyota atakayetamba zaidi baada ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## Nukuu

"Kama kesho Cristiano Ronaldo akiamka na kusema, 'nataka kwenda kucheza sehemu nyingine', nani anaweza kumnunua? Ni mzunguko uliofungwa. PSG imeingia kwenye mzunguko huo. Tunatakiwa kujiandaa kwenye dirisha la usajili na hivyo ndivyo tunavyofanya, tuna vipaumbele vyetu, orodha yetu, lakini yasiyotarajiwa yanaweza kutokea, **"Mkurugenzi wa Soka wa Klabu ya PSG, Leonardo.**



"Namjua vizuri sana [Paul Pogba] na analijua kundi lile [Man United] vizuri, kwa hali aliyonayo pale klabuni kwa sasa, hawezi kuridhika nayo na hasa muda wa kucheza na nafasi anayocheza. Kuna nyakati mambo yanakuwa magumu kwa hali fulani na unaona kabisa sehemu uliyopo haina maana tena, na hivyo ndivyo ninavyoona mambo yanavyokwenda kwa Pogba,**" Kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps.**



"Ni ligi tatu zenye aina tofauti kabisa ya soka, nilipata uzoefu mkubwa sana wa kujifunza kule Italia, moja ya shule bora kabisa kwenye suala la ulinzi, pia nilikuwa na uhusiano mzuri na (Paolo) Maldini na (Alessandro) Nesta, ambapo nilicheza nao kwa miaka miwili, hivyo nilijifunza mechi kutoka kwao, soka la Ufaransa, halitumii nguvu kubwa na PSG ni kama imetawala pale, Uingereza ni ligi inayotumia nguvu na kasi kubwa sana, iko tofauti sana na ligi hizi mbili**," beki wa Chelsea, Thiago Silva azichambua EPL, Serie A, Ligue 1.**



Nipashe
Spotika

NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 16, 2020

# KWA NINI TUNISIA HAITATOKA KWA MKAPA DHIDI YA STARS?

**Na Adam Fungamwango**

KESHO Jumanne, timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, inatupa karata nyingine itakapocheza tena na Tunisia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ijumaa iliyopita nchini Tunisia, Stars ilichapwa bao 1-0 kwenye mechi za kufuzu AFCON mwaka 2022 nchini Cameroon.

Tanzania inakamata nafasi ya tatu ikiwa na pointi tatu, ikicheza mechi tatu, ikishinda moja na kufungwa mbili, huku Tunisia baada ya ushindi huo, ikikamata usukani wa Kundi J kwa kufikisha jumla ya pointi tisa, ikishinda michezo yake yote mitatu iliyocheza.

Equatorial Guinea, baada ya kupata ushindi ugenini wa mabao 3-2 dhidi ya Libya, inakwea hadi kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu, kama Libya na Stars, lakini yenyewe ina uwiano mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa, Libya ikishika mkia kutokana na mabao mengi ya kufungwa.

Pamoja na kufungwa, Stars kwenye mechi ya kesho ina sababu kadhaa za kushinda ili kupata pointi tatu, zitakazowafikisha pointi sita kwa ajili ya kusaka tiketi hiyo...



Wachezaji wa timu ya taifa, Taifa Stars, Erasto Nyoni na Faridi Mussa (kushoto), Jonas Mkude na Salum Aboubakar, wakijipanga kumdhibiti mmoja wa washambuliaji wa timu ya Taifa ya Tunisia kwenye mechi iliyochezwa nchini humo, Ijumaa iliyopita, Stars ikilala kwa bao 1-0.

**#1. Kurekebisha makosa ya mechi iliyopita**

Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije amesema kupoteza mechi dhidi ya Tunisia kulitokana na makosa madogo madogo ambayo ameahidi kuyarekebisha kabla ya mechi nyingine. Akasema kipigo hicho kimekuwa ni somo, hivyo watapambana kwenye mechi za marudiano.

"Mechi ilikuwa kubwa na ngumu. Wapinzani wetu ni moja kati ya timu kubwa Afrika, wapinzani wetu walijitahidi kutushambulia sana, lakini na sisi tulikaa imara. Hiyo inaonyesha jinsi gani mechi ilivyokuwa ngumu pande zote mbili. Tumefungwa kwa sababu walipata penalti.

"Ulikuwa ni mchezo mgumu na wenye ushindani, tunarudi nyumbani tunaamini tutafanya vizuri na kupata matokeo chanya kwenye mchezo wetu wa marudio," alisema Ndayiragije, ikionyesha kuwa ameyaona makosa yote, hivyo kwenye mechi ya kesho kunaweza kukawa kuwapo kwa mabadiliko makubwa.

**#2. Kubadilisha mfumo wa ushambuliaji**

Iwapo Stars inahitaji kushinda mechi ya kesho, inahitaji kubadilika na kuchezesha mastraika wawili badala ya mmoja. Katika mechi ya Ijumaa, Stars ilikuwa na straika mmoja tu mbele, John Bocco ambaye pamoja na kujitahidi sana, lakini walikuwa kwenye wakati mgumu dhidi ya mabeki wawili wa Tunisia, warefu na wenye nguvu, lakini pia wakisaidiwa na kiungo mkabaji wao.

Kilichotokea ni kwamba Bocco anapoupata mpira na kuuzuia, viungo wa Stars walikuwa wazito kusogea mbele, badala yake ilionekana kama viungo wengi walihitaji zaidi kuzuia kuliko kushambulia.

**#3. Tunisia hii siyo ile**

Kingine kinachoweza kuibeba Taifa Stars kushinda mechi ya kesho ni kiwango kilichoonyeshwa na kikosi cha Tunisia kwenye mechi ya Ijumaa iliyopita. Kila mmoja aliyekuwa akiitazama mechi ile, alichokiona ni tofauti na alichofikiria. Stars ilionekana kuimudu Tunisia. Kama si goli la penalti ambalo ililipata, huenda mechi hiyo ingeisha kwa sare.

**#4. Kutokuwapo kwa Ligi Kuu Tunisia**

Mpaka sasa hakuna ligi yoyote nchini Tunisia. Ligi haijaanza kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona. Kutokuwapo kwa ligi, kumewafanya baadhi ya wachezaji wa timu hiyo kutokuwa kwenye viwango vya kawaida.

Bado wachezaji wa Tunisia wanaonekana wazito. Hawana kasi ile iliyozoeleka ya wachezaji kutoka Afrika Kaskazini, maarufu kama Waarabu. Ni wachache sana ambao wanacheza soka la kulipwa nje ya nchi ambako ligi tayari zimeshaanza. Hii ni faida kwa Stars ambayo itakuwa iko nyumbani.

**#5. Kucheza mbele ya mashabiki**

Kwa aliyetazama mechi iliyopita nchini Tunisia, inawezakana moja ya sababu iliyowafanya Watunisia kubanwa sana na Taifa Stars ni kucheza bila mashabiki. Ni ukweli usiopingika mashabiki wa soka wa Afrika Kaskazini ni 'vichaa' wa soka.


Muda wote wanashangilia na kuihamasisha timu zao. Kama hazikukufunga kimpira, basi zinaweza kuwafunga kwa kelele za mashabiki, ambao hutumia kila kitu wanachodhani kinaweza kuwatia hofu wapinzani wao kama vile fataki, tochi, kelele na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Watunisia walichokosa kwenye mechi hiyo ni sapoti kwa mashabiki wao. Kinyume chake, Taifa Stars inakwenda kucheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa na asilimia 50 ya mashabiki ambao wataruhusiwa kuingia uwanjani.

Kitendo cha kuruhusiwa mashabiki ambao wengi wao watakuwa ni Watanzania, ni faida kubwa kwenye kupata ushindi.

Mashabiki wa Stars watakaokuwa nyuma ya timu yao, watakuwa wakiishangilia timu yao mfululizo, ikicheza mbele ya Tunisia ambao inaonekana hawapo vema mwaka huu, ingawa wanaongoza Kundi J.

**JE, WAJUA?**




MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Mfaransa Thierry Henry, ni mchezaji pekee hadi sasa anayeshikilia rekodi katika Ligi Kuu England ya kufunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho (assist) 20 katika msimu mmoja wa ligi hiyo, akifanya hivyo msimu wa 2002-03.



# Wabunge wa Tanzania EALA wafundwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, amewataka wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki kutanguliza maslahi ya nchi kwenye utekelezaji wa majukumu yao. Balozi Ibuge aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na wabunge hao, jijini hapa.

Alisema maslahi ya Tanzania ni lazima yawe kipaumbele chao katika kutekeleza majukumu yao, ili kufanikisha ushiriki wa Tanzania kikamilifu kwenye mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Endeleeni kushikilia msimamo wa kutanguliza maslahi ya Tanzania siku zote, mwendelee kufanya kazi hiyo nzuri kwenye masuala mengine yote yanayogusa maslahi ya nchi yetu," alisema.

Balozi Ibuge alibainisha kuwa nafasi yao ya ubunge inatokana na uwepo wa jimbo lao ambalo ni Tanzania. Aliwahimiza kuwasiliana mara kwa mara na serikali ili kupata maoni, ushauri na msimamo wa serikali katika kujadili na kupitisha masuala mbalimbali ndani ya bunge hilo.

"Pia jiepusheni na migogoro ndani ya Bunge na Jumuiya kwani kufanya hivyo kutaiwezesha Tanzania kujiweka sawa katika nyanja za siasa na diplomasia," alisema.

Aliwapongeza namna wanavyoshughulikia muswada binafsi wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wabunge hao, Adam Kimbisa, aliishukuru wizara kwa kukutana nao kuwapa mwongozo wa namna ya kushughulikia mambo mbalimbali yanayoendelea ndani ya Bunge na Jumuiya kwa ujumla.

Alimhakikishia Katibu Mkuu huyo kuwa wabunge hao wataendelea kuhakikisha maslahi ya Tanzania yanazingatiwa katika hatua zote za mtangamano kupitia ushiriki wao katika Bunge hilo.



Mwenyekiti wa Msikiti wa Nunge, Alhaji Ismail Daud (kulia), akitoa nasaha zake kwa waumini waliohudhuria katika sherehe ya Maulidi ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mtume Muhamad (S.A.W) zilizofanyika msikitini hapo, Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Uwekezaji OSHA kupunguza malalamiko sehemu za kazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema matumizi ya vifaa vya kisasa ambavyo Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imewekeza, yatasaidia kupunguza malalamiko sehemu za kazi.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Andrew Massawe, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku mbili, yaliyoandaliwa na OSHA kwa ajili ya wakaguzi wa afya yaliyofanyika jijini hapa.

Massawe alisema matumizi ya vifaa vipya vya kisasa hususani kipimo cha macho itasaidia sana kupunguza malalamiko ya baadhi ya wafanyakazi, kutokubaliana na majibu ya vipimo ambavyo wanapatiwa.

Pia, alisema itasaidia kuwafikia watu wengi kutokana na kuwa na majibu yenye uhakika.

"Kitendo cha wakala huu kuwekeza kwenye vifaa vya kisasa ni jambo la kupongezwa na zuri, kwa mfano kifaa kinachopima macho kina uwezo wa kutambua uwezo wa macho kuona," alisema.

Aliitaka OSHA kuangalia namna pia ya kupata vifaa vya vingine vya kisasa kwenye maeneo mengine. Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema lengo la mafunzo hayo ni sehemu ya programu yao ya kuwajengea uwezo zaidi wakaguzi wa afya wa OSHA.

"Mafunzo ya leo yalikuwa maalumu juu ya matumizi ya vifaa vipya vya kupima macho ambavyo taasisi imenununua," alisema. Alifafanua kuwa vifaa hivyo vya macho ambavyo kitaalamu vinajulikana kama VT 1 master vina wigo mpana zaidi wa kutoa majibu tofauti na kifaa cha snell chart ambacho chenyewe kina uwezo wa kupima uwezo wa macho kuona mbali au karibu tu, hivyo kushindwa kubainisha tatizo jingine la macho. "Pia kifaa cha snell chart kinashindwa kutofautisha rangi, kuona usiku, kazi yetu pia ni kufanya uchunguzi wa ajali sehemu za kazi zinapotokea, tathmini ndogo tulioifanya, tuliona kuwa ajali nyingi zinazotokea sehemu za kazi, ukiwauliza wahusika wanakuambia hakuona kilichotokea," alisema.

Aliongeza: "Tukaona kwamba kumbe mtu anaweza akawa na matatizo ya macho bila yeye kujua na hivyo kusababisha ajali."

Naye Mkufunzi wa Mafunzo hayo, Dk. Robert Mazengo, alisema vifaa hivyo vya kupima macho ambavyo OSHA, imevipata ni vifaa vya kisasa zaidi, na vinauwezo mkubwa zaidi wa kubaini mambo mbalimbali ambayo yatasaidia kuwashauri waajiri.

# Majina ya walinzi kampuni binafsi kuorodheshwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPUNI za ulinzi sekta binafsi zimesema zimejipanga kuanzisha mtandao wa kuorodhesha majina ya walinzi wote nchini ikiwa ni sehemu ya kuboresha utoaji huduma za ulinzi.

Mwenyekiti wa Ulinzi Sekta Binafsi Tanzania, Felix Kagisa, aliyasema hayo baada ya kikao cha kampuni hizo kilichofanyika jijini hapa.

"Tumepanga kuanzisha mtandao wa kuorodhesha majina ya walinzi wote nchini ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa kampuni zote," alisema.

Aidha, Kagisa alisema kuwa kila mlinzi atatakiwa kuwa na kitambulisho na lengo la kuanzisha mtandao huo nchini ni kuimarisha utoaji wa huduma ya ulinzi nchini inakuwa imara.

"Baadhi ya kampuni zimeshaanza kuandikisha majina ya walinzi wao, ili kuwasilisha katika mtandao huo jambo litakalosaidia upatikanaji wa mlinzi pale panapotokea changamoto yoyote katika kituo chake cha kazi," alisema.

Kagisa pia alisema wataanzisha miradi mbalimbali ili kusaidia kampuni hizo kusimama imara na kujiendesha bila utegemezi wowote.

Alisema sasa ni wakati wa kufanya kazi ya ulinzi kama biashara, ili kuongeza kipato chao kitakachosaidia uendeshaji wa kampuni zao bila tatizo.

Kadhalika, alisema kuwa wameandaa rasimu itakayowasilishwa bungeni na kujadiliwa ili kuwa na sheria itakayoongoza kampuni hizo katika utoaji huduma hapa nchini.

Kagisa alisema wamekutana kuweka mikakati ya kusukuma maendeleo ya utendaji wao na kuangalia kero zilizopo namna ya kuzitatua ili kuleta ubora katika utoaji huduma kwa jamii.

Mwenyekiti huyo alisema walikuwa wanajiandaa na mkutano mkuu wa uchaguzi utakaofanyika mwakani mwezi wa Februari mwakani kwa kuwa kila baada ya miaka mitano wanafanya uchaguzi wa viongozi wapya.

"Tatizo kubwa katika kampuni zetu hapa nchini ni kwamba wanatoza kiwango cha chini cha fedha na kufanya sekta hiyo kuwa imara na kuleta changamoto ndogo ndogo kwa watendaji," alisema.





# Watoa huduma afya wajengewa uwezo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATAALAMU na watoa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya nchini wamejengewa uwezo wa kusoma mashine za mionzi (Utrasound), wajawazito wakati wa dharura, ili kurahisisha utendaji na kuokoa afya ya mama na mtoto aliye tumboni.

Mafunzo hayo yalitabiriwa na Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kwa kushirikiana na Shirika la "Foundation For medical Know how Transfer" la nchini Switzerland kwa kipindi cha wiki mbili, jijini hapa.

Mratibu wa mafunzo hayo kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Zacharia Amos, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha kuwapima wajawazito na kutambua umri na hali ya ukuaji wa mtoto tumboni kabla ya kujifungua.

"Tumewajengea uwezo watoa huduma mbalimbali wa vituo vya afya na hospitali nchini, ili wawe na uwezo wa vipimo vya dharura vya utrasound kwa ujauzito kuanzia wiki 20 hadi 24 kujua umri wa mimba," pamoja na matatizo mengine yanayowakabili na kuchukua hatua mapema.

Dk. Amos aliongeza kuwa ujuzi huo utawasaidia pia kutambua umri na hali ya ukuaji wa mtoto tumboni kabla ya kujifungua na endapo kutakuwa na tatizo lolote la kuokoa maisha ya mama na mtoto tumboni.

Mmoja wa wakufunzi wa mafunzo hayo, Gilbert Kraehenbuehl kutoka nchini Switzerland, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wataalamu hao kutoa huduma za dharura za kipimo cha Utrasound kwa wagonjwa walio katika hali mbaya.

Mahundi Mwasomola kutoka Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya, alisema kupitia mafunzo hayo watatoa huduma ya vipimo vya utrasound na matibabu kwa muda mfupi.

Pamoja na kuongeza ujuzi wa namna kuhuduma wajawazito wanaofika hospitalini katika hatua za mwisho za kukaribia kujifungua na kujua vihatarishi vya uzazi pingamizi kabla ya kujifungua.

Mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutumia utrasound yamefanyika kwa wiki mbili katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na kuhudhuriwa na washiriki 48 kutoa hospitali pamoja na vituo vya afya kutoka mikoa mbalimbali nchini.

# Wakulima pareto wapewa ushauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa pareto mikoa ya Mbeya na Songwe walioingia kwenye mfumo wa kilimo cha mkataba, wameshauriwa kuzalisha zao hilo kwa kufuata kanuni za kitaalamu wanazoelekezwa na wataalamu wa kilimo ili kuongeza ubora na thamani.

Wakulima hao wametakiwa kukausha mazao yao kwa kutumia mbinu za kitaalamu hasa mabani (vibanda vya kukaushia) ya kisasa ambayo yanatumia nishati kidogo ili kuhakikisha pareto zao zinakuwa na kiwango cha sumu kinachotakiwa.

Msimamizi wa kilimo cha zao hilo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mussa Malubalo, alisema kwa sasa wameanza mikakati maalumu ya kuboresha kilimo hicho katika mikoa yote inayozalisha zao hilo kwa kuanzia na Mbeya na Songwe.

Alisema mikakati wanayoifanya ni pamoja na kutoa elimu ya kitaalamu ya uzalishaji wa zao hilo ambalo ni miongoni mwa mazao makubwa ya biashara kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe hasa katika wilaya tatu ambazo ni Mbeya, Rungwe na Ileje.

Alisema katika kuhakikisha zao hilo linakuwa la kimkakati, wamefanikiwa kuwaunganisha wakulima zaidi ya 10,000 katika vikundi lengo likiwa kuwafikia 13,000 ambao tayari wanaendelea kunufaika kwa kupatiwa elimu na pembejeo.

"Serikali imeelekeza nini cha kufanya katika kusaidia wakulima wa mazao mbalimbali yaliyopewa kipaumbele, lengo ni kuwawezesha kuzalisha mazao yaliyo na ubora na kupata masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi," alisema Malubalo.

Mtaalamu wa kilimo cha pareto anayesimamia mikoa ya Mbeya na Songwe, Suleiman Juma, alisema asilimia 87 ya kilimo hicho kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe ina ubora na ndiyo inayotegemewa nchini.

Alisema pareto hiyo ina soko la uhakika kutokana na ubora wake na unapimwa kutokana na kiwango cha sumu kilichomo.

"Tumefikia hatua hiyo baada ya kupata maelekezo ya serikali na hivyo kuwa na mfumo wa kilimo mkataba kwa wakulima kwa kuwaunganisha kwenye vikundi, tunawapatia elimu ya namna ya kuhudumia zao hilo kuanzia hatua ya uoteshaji miche, palizi mpaka ukaushaji," alisema Juma.

Naye Mratibu wa zao hilo, Mkoa wa Mbeya, Michael Bishubo, alisema tangu kuanza kwa mfumo huo uzalishaji umeongezeka kutoa tani 13,000 za awali mpaka 19,000 katika msimu wa kilimo wa 2019/2020 na mkakati ni kuongeza tija zaidi ya uzalishaji nchini.

Alisema pamoja na ongezeko la uzalishaji, pia bei imeongezeka kutoka Sh. 2,000 kwa kilo mpaka kufikia Sh. 2,300 na kuna uwezekano bei hiyo ikapanda zaidi ya hapo misimu ijayo.

Baadhi ya wakulima waliiomba serikali kudhibiti kampuni za ununuzi kuwa na mfumo endelevu ambao utaleta tija kwa wakulima na wanunuzi wanaowapunja wakulima.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Saimon, akikagua gwaride lililoandaliwa na vijana wa Mgambo wakati wa kufunga mafunzo yao, mwishoni mwa wiki katika Kata ya Kiwanja wilayani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba udhibiti bei ya mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa mahindi katika Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kudhibiti wauzaji wa mbolea ili wasipandishe bei na kusababisha gharama za uzalishaji kuongezeka na kuwa juu kuliko bei wanayouza mazao yao baada ya mavuno.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima hao walisema bei ya mbolea huwa inapanda bila utaratibu hasa mvua ikianza kunyesha na kuiomba serikali kuwafikishia bidhaa hiyo mapema, ili kuepuka tatizo hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Stephano Mwalugombo, Kijiji cha Ilota, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema wafanyabiashara wanapandisha bei kwa kisingizio cha kuongezeka gharama za usafirishaji kutokana na ubovu wa barabara hasa maeneo ya vijijini.

Alisema wakati mwingine wafanyabiashara hao huwa wanasafirisha mbolea pamoja na pembejeo zingine mapema kabla ya mvua na kuzihifadhi mpaka mvua ianze kunyesha ndiyo waanze kuuza kwa bei ya kuruka. "Sisi huwa tunalazimika kufuata mbolea Mbalizi ambako ni zaidi ya kilomita 20, lakini ni bora uende kununua Mbalizi usafirishe kwa baiskeli kuliko kununua hapa kwa wafanyabiashara wetu kwa sababu huwa wanatuumiza sana. Alisema wakati mwingine katika maeneo yao huwa ni vigumu kujua bei elekezi zinazotolewa na serikali kutokana na mawasiliano kuwa magumu.

Naye Sarafina Myombe, alisema kwa sasa wananunua mbolea ya kupandia kwa bei ya kati ya Sh. 58,000 na 60,000, lakini mvua ikianza kunyesha wanauziwa kwa Sh. 70,000.

Aliiomba serikali kutumia utaratibu wa kutuma ujumbe mfupi wa simu kwa wananchi unaoelezea bei elekezi ya pembejeo kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi ambalo alidai huwa linatoa tahadhari mbalimbali kwa wananchi kuhusu usalama wa fedha kwa kutumia jumbe za aina hiyo.



# Wamiliki wa magari wapewa angalizo nyaraka zisizo rasmi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAMILIKI wa magari ya biashara wametakiwa kuacha tabia ya kujitafutia nyaraka ambazo hazikutolewa na mamlaka zinazohusika na kuzitumia kufanyia biashara ya kusafirishia abiria.

Onyo hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi na Usalama Barabarani kutoka Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mohamed Simba Hassan, alipokuwa akizungumza na wadau wa sekta ya usafiri mjini hapa.

Simba alieleza kuwa serikali ilishazuia uingiaji wa gari aina ya dungu na kuzuiliwa kusajiliwa kufanya biashara ya daladala badala yake magari yaliyokuwapo yaendelee kutumika hadi yatakapochakaa.

Alisema kwa sasa wamejitokeza baadhi ya watendaji wasio waaminifu wanaoingiza magari hayo na kuyapatia usajili wa nambari za zamani, ili yaonekane kuwa ni ya zamani na kuyahalalisha bila ya kufuata utaratibu.

Aidha, aliwaonya wasimamizi wa ruti wanaojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa sheria za barabarani pamoja na kuruhusu magari binafsi kuchukuwa abiria, kuuza zamu pamoja na kuruhusu kutowafikisha abiria mwisho wa ruti kuacha mara moja vitendo vya aina hiyo.

Aidha katika kikao hicho, Simba alielezea mikakati ya mamlaka ya usafiri na usalama barabarani kuwa katika kipindi hiki mamlaka haitosita kumchukulia hatua kali za kisheria na kinidhamu dereva yeyote atakaebainika akivunja sheria za usafiri barabarani.

Alisema dereva atakayepatikana akisababisha ajali za kizembe barabarani mbali ya kupelekwa katika vyombo vya sheria, mamlaka itamfanyia mitihani ya udereva na ikibainika kutozifahamu sheria za barabarani, hatua za kupunguza daraja au kufuta leseni yake dereva huyo zitachukuliwa. Sambamba na hilo, Simba pia alieleza kuwa wamiliki wa magari ya abiria wanamchango mkubwa wa kuisimamia sekta ya usafiri barabarani, hivyo wana wajibu wa kuunga mkono juhudi za serikali za kusimamia usafiri huo, ili kupunguza ajali za barabarani.

Akizungumzia suala la ukaguzi wa vyombo vya moto, alieleza kuwa kuanzia leo mamlaka itaendeleza ukaguzi wa vyombo vya moto barabarani pamoja na kutoa elimu ya usalama barabarani katika vijiwe na vituo vya magari ya abiria, utekelezaji wa utaratibu huo ulikuwa umesitishwa kupisha uchaguzi mkuu wiki chache zilizopita.

Simba aliwaomba wananchi wote kuripoti vitendo vya udhalilishaji na ukiukwaji wa sheria za barabarani kwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ili hatua kali ziweze kuchukuliwa.

Wadau wa sekta ya usafiri walisema hivi sasa kumekuwa na kikwazo cha Jeshi la Polisi kusimamisha magari katika sehemu zisizo rasmi, hali ambayo inaweza kusababisha ajali.



Ofisa wa kitengo cha maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Zuhura Saleh, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maradhi hayo.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Kusini Unguja watekeleza agizo la Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKOA wa Kusini Unguja umeanza kutekeleza kwa vitendo hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyoitoa wakati akizindua Baraza la 10 la Wawakilishi kwa kuanza shughuli za usafi katika maeneo mbalimbali ya kijamii ikiwamo masoko na vituo vya afya.

Akizungumza baada ya zoezi hilo, Mkuu wa Mkoa huyo, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema suala la usafi lina umuhimu wa kipekee katika kufikia uchumi wa bluu.

Alisema ili kufikia azma hiyo ipo haja ya kuweka hali ya usafi katika maeneo ya biashara, taasisi za serikali na binafsi pamoja na maeneo ya utalii.

Aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya wilaya hadi shehia kuhamasisha na kusimamia wananchi katika kuhakikisha wanaitumia siku ya Jumamosi ya kila wiki kufanya usafi katika maeneo yao.

"Mazingira yakiwa safi huvutia watalii wengi kufika na serikali kupata mapato," alisema Ayoub.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kati, Kihamida Mussa Khamis na Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Idrisa Kitwana Mustafa, waliahidi kusimamia zoezi hilo na kuhakikisha linakuwa endelevu kwa kufanya ukaguzi katika maeneo tofauti kila Jumamos ili kuwabaini watakaokaidi agizo hilo.

Wananchi walioshiriki katika zoezi hilo walisema hatua iliyochukuliwa na uongozi wa mkoa huo, itasaidia kupunguza au kuondosha hali ya uchafu, jambo ambalo litasaidia kuepukana na magonjwa mbalimbali yakiwamo ya mlipuko.

# Sababu wanaume kupoteza nguvu za kiume zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUPOTEZA nguvu za kiume na hamu ya kushiriki katika tendo la ndoa kwa wanaume kumeelezwa ni moja ya athari za maradhi yasiyoambukiza ikiwamo ugonjwa wa kisukari.

Hayo yalielezwa jana na ofisa kutoka kitengo cha maradhi yasioambukiza Zanzibar wakati akizungumza katika mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu maradhi yasiyoambukiza yaliofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema kuwa idadi ya wagonjwa wa maradhi yasioambukiza Zanzibar yameongezeka na kusababisha baadhi ya wanaume kupoteza hamu ya kushiriki katika tendo la ndoa.

Alisema sababu ya maradhi yasioambukiza haijajulika isipokuwa kuna vichocheo vinavyosababisha kuongezeka kwa wagonjwa wa maradhi hayo.

Alivitaja baadhi ya vichocheo hivyo ni baadhi ya vichocheo haviepukiki ikiwamo urithi na umri mkubwa.

Alisema baadhi ya watu wanapata magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, saratani na ugonjwa wa moyo kutokana na urithi au umri kuanzia miaka 40 na kuendelea.

Aidha, alivitaja vichocheo ambavyo vinaepukika ni matumizi ya pombe, tumbaku, uvutaji sigara na uzito mkubwa.

Alisema ili kuepukana na maradhi hayo ni vyema kuepuka kunywa pombe, kutovuta sigara, kutokula tumbaku na kufanya mazoezi.

Naye mshauri nasaha wa kitengo cha maradhi yasiyoambukiza, Rabia Ali Makame, alisema asilimia 18 ya wananchi wa Zanzibar ndio wanaofanya mazoezi ambapo idadi kubwa hawafanyi mazoezi na kupelekea kupata magonjwa ya maradhi yasiyoambukiza.

Alisema madhara ya magonjwa hayo hupelekea msongo wa mawazo, vifo vya ghafla, kupata ulemavu wa kudumu kutokana na kukatwa viungo vya mwili hasa kwa wagonjwa wa kisukari na saratani.

Alisema wanaume wapo katika hatari zaidi ya kupata magonjwa yasioambukizwa ikilinganishwa na wanawake kutokana na wanaume hubaki na matizo yanayowakumba bila ya kumweleza mtu mwingine tofauti na wanawake.

"Wanawake wanapokuwa na jambo linamkereketa hupenda kumweleza mtu mwingine, hali hiyo inasaidia kutokuwa na kinyongo rohoni tofauti na wanaume ambao wao huwa wanabaki nayo wenyewe na hupelekea kuwa na msongo wa mawazo na hatimaye kupata maradhi yasiyoambukiza," alisema.

Aidha, alisema wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari Zanzibar wanavuta sigara, hali ambayo itapelekea kupata maradhi yasioambukiza kutokana na moshi wa sigara ambao ni hatari kwa afya zao.

# Wafuasi Trump waandamana wakidai kuibiwa kura

**WASHINGTON, Marekani**

MAELFU ya wafuasi wa Rais Donald Trump wameandamana jijini Washington, kumuunga mkono kiongozi huyo anayemaliza muda wake.

Maofisa wa Marekani wametupilia mbali madai ya Rais Trump ya kutokea udanganyifu katika uchaguzi wa Novemba 3.

Waandamanaji hao walikuwa wakiimba nyimbo za kudai kiongozi huyo anafaa kuendelea kubakia madarakani kwa miaka mengine minne.

Rais Trump na wafuasi wake wanadai kwamba, kulifanyika udanganyifu kwenye uchaguzi mkuu wa Novemba 3, uliopelekea rais huyo kushindwa na Rais mteule Joe Biden, na kulazimika kuondoka Ikulu baada ya muhula mmoja tu madarakani.

Rais Trump binafsi na msafara wake wa magari alipita katikati ya maandamano hayo akiwa njiani akielekea kwenda kucheza gofu, huku wafuasi wake wakimshangilia naye akiwaonyesha tabasamu.

Watu wasiopungua 10,000, ambao wachache walikuwa wamevaa barakoa, walikutana katika ukumbi wa Freedom Plaza, kabla ya kuandamana hadi katika Mahakama Kuu, huku wakipeperusha bendera za kumuunga mkono Rais Trump.

"Tulitaka kumwonyesha kuwa tunamuunga mkono, tunahisi wanajaribu kuiba uchaguzi," alisema Pam Ross, akimaanisha wapinzani wa kisiasa wa Rais Trump, ambaye aliendesha gari kwa saa nane kutoka Ohio kushiriki maandamano hayo.

Kiongozi huyo wa Republican anashikilia madai yake kwamba kulifanyika udanganyifu na kwamba alimshinda Biden katika uchaguzi wa Novemba 3.

Rais Trump aliandika ujumbe kadhaa katika mtandao wa kijamii wa Twitter, zenye madai kwamba mashine za kuhesabia kura zilikuwa zimedukuliwa na kwamba vyombo vya habari vilikuwa na hitilafu katika jinsi vilivyotangaza taarifa za uchaguzi huo. **DW**




Maelfu ya wafuasi wa Rais wa Marekani, Donald Trump, wakiwa wameandamana jijini Washington kumuunga mkono kiongozi huyo anayemaliza muda wake. **PICHA: REUTERS**

# Mapigano Ethiopia, viwanja vya ndege vyashambuliwa

**ADDISABABA, Ethiopia**

WANAJESHI katika Jimbo la Tigray lililopo Kaskazini mwa Ethiopia wamefyatua mabomu katika jimbo jirani, kwenye mzozo wao na serikali ya Ethiopia unaoendelea kupanuka.

Hali ya uhasama baina ya serikali na wanajeshi wa Tigray People's Liberation Front (TPLF), wanaodhibiti jimbo hilo, ilitokota na kusababisha makabiliano ya kijeshi mwezi huu.

Maofisa wa jeshi walisema maeneo ya viwanja vya ndege yameharibiwa katika shambulio la mabomu. TPLF walithibitisha kuhusika, wakisema kuwa mashambulio yalikuwa ni ya ulipizaji kisasi.

Shirika la ya kutetea haki za binadamu la Amnesty International limesema limethibitisha kwamba watu wengi wameathirika na huenda mamia ya watu, walichomwa visu au kukatwa mapanga hadi kufa katika mji wa Mai-Kadra (May Cadera) mwanzoni mwa mwezi huu.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed amewashutumu vikosi vinavyowatii viongozi wa Tigray kwa kufanya mauaji ya watu wengi, lakini TPLF wamekanusha kuhusika.

Abiy aliamuru kufanyika kwa harakati za kijeshi dhidi ya TPLF mapema mwezi huu, baada ya kuwashutumu kushambulia kambi ya kijeshi ya wanajeshi wa shirikisho - madai yanayokanushwa na TPLF.

Mapigano hayo mabaya yamewalazimisha maelfu ya raia kuvuka mpaka na kuingia nchi ya Sudan, ambayo inasema itawapatia hifadhi katika kambi ya wakimbizi.

Taatifa zaidi zinaeleza kuwa hali ya kisiasa katika Jimbo la Tigray mbaya na kwamba kwa sababu huduma ya mtandao haipatikani kwa urahisi.

Wakati huohuo, Kikosi kazi cha dharura cha serikali ya Ethiopia kilisema mabomu yalifyatuliwa kuelekea katika miji ya Bahir Dar na Gondar, katika Jimbo la Amhara, Ijumaa jioni.

Ofisa mmoja wa Jeshi la Ethiopia aliliambia Shirika la habari la Reuters kwamba bomu moja lilipiga uwanja wa ndege uliopo Gondar na kuuharibu kidogo, huku la pili lilianguka tu nje ya uwanja wa ndege wa Bahir Dar.

Viwanja hivyo vyote vya ndege hutumiwa na ndege za kijeshi pamoja na za raia.

Vikosi kutoka Amhara vimekuwa vikipigana sambamba na vikosi vya serikali kuu ya shirikisho dhidi ya wapiganaji wa Tigray.

TPLF imesema kuwa shambulio la bomu lilikuwa ni la kulipiza kisasi kwa shambulio la hivi karibuni lililofanywa na vikosi vya Abiy.

Shambulio la bomu limeibua hali ya wasiwasi kwamba mapigano katika jimbo la Ethiopia lililoko kaskazini yanaweza kusambaa katika maeneo mengine ya nchi. **BBC**

# Simu bei 'chee' kurahisisha uhamiaji teknolojia ya 4G

**JOHANESBURG, Afrika Kusini**

IMEELEZWA kuwa urahisishwaji wa upatikanaji wa simu janja kwa bei rahisi ni miongoni mwa njia mahususi zinazoweza kuchochea uhamiaji kuelekea matumizi ya teknolojia za 4G na 5G barani Afrika.

Ujumbe huo umebainishwa kupitia mkutano wa tano kuhusu mawasiliano ya mtandao barani Afrika wa Huawei uliofanyika kuanzia Novemba 9 hadi 12, mwaka huu.

Ilielezwa kwamba tasnia ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (ICT), haijaweza kuwa umuhimu zaidi kwa jamii, na kwamba kwa sasa tasnia hiyo ipo mstari wa mbele katika kuleta maendeleo ya kijamii na kurejesha uchumi ulioathiriwa na ugonjwa wa virusi vya corona.

"Muunganiko kupitia teknolojia ya mawasiliano ni msingi wa mabadiliko ya kuelekea ulimwengu wa kidigitali," alisema Dk. Mohamed Madkour, Makamu wa Rais, Biashara Masoko na Ufumbuzi kutoka kampuni ya Huawei.

Kwa mujibu wa ripoti ya GSM, idadi ya watumiaji wa mtandao wenye kasi ya 4G barani Afrika inatarajiwa kuongezeka mara tatu katika miaka mitano ijayo, huku idadi ya watu ikitarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 55 hadi 80 ifikapo mwaka 2025.

"Uunganishaji wa ulimwengu barani Afrika unahitaji ushirikiano thabiti kutoka kwa wadau wote, ili kukuza biashara zenye faida na pia kuhimiza uwekezaji," alisema Madkour.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara ya Ng'ambo kutoka moja ya kampuni zinazotengeneza, Roy Zheng, alisema tangu kuanza kwa ugonjwa wa corona, mahitaji ya vifaa hivyo vinavyotumika kutoa elimu yaliongezeka.

Alisema ili kukidhi mahitaji hayo, kampuni yake ilikuwa ikitoa 'chipsets' ambazo zinawezesha utengenezaji wa vifaa hivyo kwa bei iliyoanzia Dola za Kimarekani 48.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu ya Tele 1, Lin Ranhao, alisema katika miaka ijayo, ukuaji wa haraka zaidi wa wigo wa watumiaji wa 4G unatarajiwa kutoka barani Afrika.

Alisema Afrika ina watumiaji wengi wa 2G wanaosubiri kubadili kuelekea 4G, lakini licha ya miundombinu iliyo tayari, upenyaji wa 4G bado uko taratibu.

Ranhao alisema mipango ya ruzuku pamoja na uuzaji wa simu janja kwa bei ndogo vitapunguza changamoto kwa wanunuzi wa kwanza wa simu janja, kuharakisha uhamiaji wa 4G na kufungua fursa kubwa kwa biashara na kwa maendeleo ya binadamu. **VOA**

HABARI MICHEZO

# MESSI

## ANA SABABU KUONDOKA BARCA - FIGO




**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi atakuwa na malengo na sababu za kutaka kuondoka Barcelona na hakuna kitakachoweza kuzuia maamuzi yake, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa klabu hiyo, Luis Figo.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, aliishtua dunia Agosti mwaka huu wakati alipoitaarifu Barca mpango wake wa kutaka kuondoka klabuni hapo ambapo amekaa kwa miongo miwili.

Lakini Figo, ambaye alishangaza kwa uhamisho wake wa utata kutoka Barca kwenda kwa wapinzani wao, Real Madrid mwaka 2000, anaamini Messi sasa akili yake inamfanya atake kuondoka pale Catalunya.

"Niliona kitu kwa Messi na jaribio lake la kutaka kuondoka Barcelona kipindi cha majira ya joto, kama ilivyo kwa mashabiki wa soka, walishituka na kushangaa," alisema akiliambia gazeti la Marca.

"Atakuwa na malengo na sababu za kufanya maamuzi yake. Sijui nini kilitokea kwake.

"Kila timu inamtaka mchezaji kama Messi, lakini hilo linategemea na hali ya kifedha kama ilivyo sasa kwa klabu, fedha atakazoigharimu klabu kwa mshahara, na nia ya mchezaji.

"Lakini kwa kawaida, kwenye maisha, kama hutaki kwenda popote, mwishoni hakuna kitakachobadilisha akili yako."

Messi mwenye umri wa miaka 33, atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, amekuwa na mwanzo mbaya msimu huu 2020-21.



## MBAPPE SASA FITI KUIVAA SWEDEN

**LISBON, Ureno**

DIER Deschamps amethibitisha Kylian Mbappe atakuwa fiti kwenye mchezo wa Ufaransa dhidi ya Sweden baada ya kuingia hatua ya fainali ya mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Mbappe alikosa mchezo wa Jumamosi wa ushindi wa 1-0 dhidi ya Ureno pale jijini Lisbon, pia akiwa amewekwa benchi kwenye mchezo wa kirafiki waliofungwa na Finland kutoka na maumivu ya misuli.

Hata hivyo, Ufaransa iliingia hatua ya fainali ya michuano hiyo, na sasa Mbappe atakuwapo kwenye mchezo wa kesho Jumanne dhidi ya Sweden.

"Atakuwapo, anaonyesha yupo tayari," alisema Deschamps.

Ufaransa imecheza mechi mbili kati ya tisa za Ligi ya Mataifa ya UEFA bila Mbappe, ikishinda zote na kufunga mabao matano.

Wakiwa na nyota huyo wa Paris Saint-Germain, wameshinda nne kati ya saba huku wakifunga bao moja kwa kila mchezo.

Bao la N'Golo Kante la dakika ya 53 liliipa ushindi dhidi ya Ureno na kuongoza Kundi lao la A3 na kutinga hatua ya fainalli ya makundi.

## KOCHA URENO AJITETEA KUMWACHA BENCHI JOTA

**LISBON, Ureno**

FERNANDO Santos ametetea uamuzi wake wa kumwanzisha Diogo Jota benchi wakati Ureno ikifungwa na Ufaransa kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Bao la N'Golo Kante la dakika ya 53 lilitosha kuwapa ushindi Ufaransa Jumamosi na kuongoza Kundi la A3 na kupata nafasi ya kutinga fainali ya makundi.

Santos aliamua kuwachezesha nyota watatu mbele, Cristiano Ronaldo, Bernardo Silva na Joao Felix mjini Lisbon, huku Jota akiingia muda mchache baada ya Kante kufunga bao.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool alitoa pasi nane zikiwa nyingi zaidi kuliko za Silva aliyecheza kwa dakika 72, lakini alimaliza bila kupiga shuti langoni.

Lakini kocha Santos alisema baada ya mchezo huo kuwa mashambulizi hayakuwa tatizo kwa Ureno kwenye mchezo huo dhidi ya Ufaransa, akitetea uamuzi wake wa kumuacha benchi, Jota.

"Kama nilivyosema kabla, timu ilicheza vizuri dhidi ya Ufaransa. Na sikumbuki mtu kuniuliza mimi kwa nini Diogo Jota hakuanza kwenye mchezo huo," alisema kocha huyo akiwaambia waandishi wa habari.

"Jota ni mchezaji wa daraja bora kabisa, kila mmoja anajua hilo. Sawa na Bernardo na pia Cristiano.

"Na Felix pia. Kama Jota angecheza na kiwango cha timu kisingekuwa bora, mngeniuliza tena kwa nini Bernardo au Felix hawakucheza. Hiyo ni kawaida."






# FERNANDES: UNITED ITATWAA UBINGWA EPL

**LISBON, Ureno**

BRUNO Fernandes hajali kama watu wanafikiri kwamba timu nyingine ni imara zaidi kuliko Manchester United, na anaamini wana nia ya kushinda mataji.

United haijashinda taji lolote tangu walipotwaa ubingwa wa Ligi ya Europa na Kombe la Ligi mwaka 2017 chini ya Jose Mourinho.

Fernandes, ambaye aliwasili pale Old Trafford Januari, aliisaidia United kutinga nusu fainali ya Kombe la FA na Europa msimu uliopita, pamoja na kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

Matumaini ya klabu hiyo kumaliza miaka nane ya kusubiri kushinda taji la Ligi Kuu, yanaonekana kuwa magumu baada ya kupoteza mechi tatu kati ya saba msimu huu.

Ushindi dhidi ya Everton kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa ulizima presha kwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Akizungumza na tovuti ya Man United, Fernandes amesema: "Kwa upande wangu, haijalishi kuhusu timu nyingine, watu wanaweza kusema wao ni bora kushinda sisi, wana 11 bora kuliko sisi, watu wanaotoka benchi ni bora kuliko sisi.

"Waache waseme wanavyofikiri wao, sijali. Kwa upande wangu, nimekuja Manchester kushinda mataji. Nacheza katika moja ya klabu kubwa duniani.

"Klabu hii imeweka historia hapo nyuma na historia ya kuvutia sana.

"Kwa klabu kama Manchester United, ni muda mrefu tangu tumeshinda taji la Ligi Kuu. Ni muda mrefu sana, nafikiri."

## ENRIQUE AJITETEA SARE HISPANIA

**BASEL, Uswisi**



LUIS Enrique ametetea uamuzi wake wa kuanza bila safu ya ushambuliaji iliyokamilika kwa Hispania wakati walipohitaji bao la dakika za mwisho kupata sare ya 1-1 kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Uswisi, Jumamosi.

Hispania walikuwa wanaelekea kupoteza mchezo mfululizo katika Kundi lake la A4 kabla ya Gerard Moreno aliyetokea benchi kusawazisha bao la Remo Freuler la kipindi cha kwanza kwenye mchezo huo ambao Sergio Ramos alikosa penalti mbili.

Akiwa ameanza na Gerard na Alvaro Morata kwenye mchezo wa kirafiki wa Jumatano dhidi ya Uholanzi, Luis Enrique alimtumia Dani Olmo pekee kuongoza mashambulizi pale kwenye dimba la St Jakob-Park.

Alikuwa straika wa Villarreal, Gerard ambaye alitengeneza tofauti kwenye mchezo huo wa kusaidia sare hiyo.

Enrique ambaye kikosi chake kimefunga mabao matatu katika mechi tano zilizopita, aliamua kuwaacha benchi Morata na Gerard hadi kipindi cha pili pale mjini Basel.

"Soka linaweza kuwa kama hivyo," alisema. "Ulikuwa mchezo wa kuvutia, lakini kuna wakati unatakiwa kusubiri ili kuweza kupata pointi moja.

"Tuliamua kwamba, namba tisa hakuwa muhimu katika kipindi cha kwanza. Tulikosa uimara na nafikiri Uswisi walikuwa bora zaidi."



## WERNER AFUNGUKA KUTUPIA MAWILI

**LEIPZIG, Ujerumani**

TIMO Werner alifurahishwa kurudi mjini Leipzig kwa kufunga mara mbili wakati Ujerumani ikishinda 3-1 dhidi ya Ukraine, Jumamosi.

Baada ya Leroy Sane kufuta lile la ufunguzi la Roman Yaremchuk pale kwenye Uwanja wa Red Bull Arena Leipzig, Werner alifunga mara mbili na Ujerumani ikapaa kileleni mwa Kundi lake la A4 kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Werner, mfungaji wa wakati wote wa Klabu ya RB Leipzig, aliondoka kwa miamba hao wa Bundesliga na kujiunga na Chelsea, Juni.

Mshambuliaji huyo aliridhishwa na mabao yake mawili hayo na kusema Ujerumani inazidi kuwa bora.

"Bao langu la kwanza kwa hakika lilikuwa rahisi kwa sababu ya pasi ya mwisho kutoka kwa Leon (Goretzka) ilikuwa nzuri, nzuri sana," alisema Werner akiiambia DFB.de.

"Kufunga mabao mawili mjini Leipzig, sehemu ambayo nilikuwa na miaka mizuri ya kuvutia, hakika ni hisia nzuri.

"Mara zote nafurahia kurudi Leipzig. Ni aibu kwamba hatukuwa na shabiki yeyote uwanjani.

"Kwa ujumla tulikuwa katika kiwango bora. Kiwango chetu kinaimarika na mambo yanaonekana kuwa mazuri. Pia tunazidi kuwa imara.

"Tunajituma ili tuweze kufanya vizuri kwenye mashindano ya Euro mwakani."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS AVUNJA REKODI YA BUFFON MECHI TAIFA

Sasa abakiza nane kuifikia rekodi ya dunia inayoshikiliwa na Hassan wa Misri, ambaye...

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos ameweka historia ya kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa timu ya taifa barani Ulaya na kuipiku ile ya gwiji wa Italia, Gianluigi Buffon.

Mlinzi huyo wa kati wa Real Madrid alifikisha mechi 177 kuichezea Hispania wakati ikitoka sare na Uswisi kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa, Jumamosi.

Hiyo inamaana kwamba, Ramos, ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia na Hispania, sasa amepitwa mechi nane tu na Ahmed Hassan wa Misri anayeshikilia rekodi ya kuichezea timu ya taifa mechi nyingi zaidi duniani.

Pamoja na kushinda Kombe la Dunia kule Afrika Kusini mwaka 2010, Ramos ameshinda mataji mawili ya Ulaya akiwa na Hispania na kufunga mabao 23 kwa nchi yake akishika nafasi ya nane kwenye orodha ya ufungaji sawa na Alfredo Di Stefano.

Zaidi ni kwamba, Ramos ndiye mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi za ushindi (129) kwa kikosi cha Hispania.

Ramos amecheza mechi nyingi zaidi dhidi ya Italia (mara 10) kuliko mchezaji yeyote wa Hispania na zote akicheza wakati Buffon akiwa golini, akishinda nne na kupoteza moja tu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amecheza mechi 17 kwenye Kombe la Dunia na 15 katika michuano ya Ulaya, wakati 97 kati yake akicheza chini ya kocha, Vicente Del Bosque, akishinda asilimia 76.2 ya mechi zote chini ya kocha huyo wa zamani wa Madrid.

Ramos alianza kucheza soka la kimataifa mwaka 2005 dhidi ya Chile.

Buffon aliweka rekodi ya kuichezea mechi nyingi zaidi Italia, wakati alipotokea benchi dhidi ya Argentina, Machi 2018, akianza kuichezea Oktoba mwaka 1997 dhidi ya Urusi.

Mkali huyo wa Juventus ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia, amecheza mechi 68 bila kuruhusu bao.

## KWA UFUPI

**MESSI ATOA SHARTI KUTUA CITY**

LIONEL Messi anataka kwanza kuhakikishiwa kama Manchester City itambakiza kocha Pep Guardiola na straika, Sergio Aguero ili aweze kutua pale, Etihad. ***(El Chiringuito via Mirror)***

**GUARDIOLA KUONGEZA MKATABA**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, mwenye umri wa miaka 49, anakaribia kuongeza mkataba wake wa miaka mitano ili kubaki klabuni hapo. ***(Telegraph)***

**CHELSEA, LIVER KWA BALDE**

CHELSEA na Liverpool zote zinafikiria kumsajili kinda wa Barcelona, Alejandro Balde, mwenye umri wa miaka 17, huku mlinzi huyo wa kushoto akitarajiwa kuingizwa katika kikosi cha kwanza na kocha Ronald Koeman. ***(Sport via Express)***

**CITY BADO YAMUWINDA MESSI**

MANCHESTER City imebaki bado ikiwa na nia ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi wakati mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Mundo Deportivo)***

**OVERMARS KUONDOKA AJAX**

MKURUGENZI wa soka wa Ajax na winga wa zamani wa Arsenal, Marc Overmars, amesema yupo tayari kupata changamoto mpya pamoja na Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Edwin van der Sar, huku wawili hao wakihusishwa na uwezekano wa kwenda Manchester United. ***(Mirror)***

**BREMER AWANIWA EPL**

KLABU za Liverpool na Everton zinawania kumsajili mlinzi wa kati wa kimataifa wa Brazil, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 23 anayecheza pale Tolino. ***(Liverpool Echo)***

**UNITED YAMWONYA BAILLY**

MANCHESTER United imemwonya wakala wa Eric Bailly kwamba, mlinzi huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 26, atahitaji kuangalia majaliwa yake kama hali ya sasa haitaimarika. ***(Calciomercato via the Sun)***

**FERNANDES KUONDOKA SPURS**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesema kiungo, Gedson Fernandes mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza kwa mkopo klabuni hapo kutoka Benfica, muda wake unaweza kumalizika Januari. ***(Sport TV via Sky Sports)***

**JUVE YAONGOZA KWA ALABA**

JUVENTUS inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, mwenye umri wa miaka 28, raia wa Austria, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Tuttosport)***

**EVERTON KUMTOSA JEAN-PHILIPPE**

KIUNGO wa Everton raia wa Ivory Coast, Jean-Philippe Gbamin, mwenye umri wa miaka 25, anaweza kuondoka klabuni hapo kwa mkopo Januari baada ya kushindwa kuwa na nafasi pale Goodison Park. ***(Football Insider via Teamtalk)***

**PHILLIPS AKARIBIA ENGLAND**

KIUNGO wa Leeds na England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 24, amesema mshambuliaji mwenzake klabuni hapo, Patrick Bamford, mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kujiunga naye kupata nafasi ya kucheza mechi za kimataifa. ***(Yorkshire Evening Post)***

**DALGLISH MATUMAINI KWA KLOPP**

GWIJI wa Liverpool, Sir Kenny Dalglish, anaamini kocha wa sasa wa 'Wekundu' hao wa Anfield, Jurgen Klopp, atapata suluhisho kwenye safu ya ulinzi baada ya kuumia kwa Virgil van Dijk na Joe Gomez. ***(Liverpool Echo)***

# MSUVA: WYDAD NJIA YA KUNIPELEKA ULAYA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA machachari wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Simon Msuva, amethibitisha rasmi kujiunga na klabu kubwa nchini Morocco ya Wydad Casablanca, akidai kuwa amefanya hivyo kwa ajili ya kutimiza ndoto alizokuwa nazo kwa muda mrefu za kuchezea klabu kubwa Afrika, ikiwa ni njia ya kuelekea barani Ulaya.

Akizungumza baada ya kuwasili nchini akitokea Tunisia akiwa na kikosi cha Taifa Stars, kitakachoshuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho dhidi ya Watunisia hao, Msuva alisema amejiunga na miamba hiyo kwa mkataba wa miaka minne na nusu akitokea klabu ya nchini Morocco pia, Difaa El Jadida.

Alisema kilichompeleka huko ni maslahi, lakini Wydad ni moja kati ya timu bora barani Afrika ambayo hushiriki vema kila msimu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na kufika mbali, na hata kuutwaa ubingwa, hivyo kuwapo kwake kwenye klabu hiyo kutamfanya kuonekana zaidi na kujitangaza ndani na nje ya bara la Afrika.

"Kabla ya kujiunga na Wydad nilipata ofa nyingi, lakini hazikuwa na maslahi mazuri kwangu, kama unavyofahamu soka ndilo linaloendesha maisha yangu ni muhimu kuangalia maslahi kwanza.

Yote kwa yote namshukuru Mungu, kikubwa niwaahidi Watanzania kuendelea kupambana bila ya kukata tamaa ili kufanikisha malengo yangu," alisema Msuva.

Msuva alijiunga na Difaa El Jadida akitokea Yanga mwaka 2017, na kabla ya hapo alikuwa akiichezea Moro United kuanzia 2011 mpaka 2012, aliposajiliwa na Yanga.

Mchezaji huyo ameshawahi kuwa mfungaji bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mara mbili kwenye misimu tofauti, 2014/15 akitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa mabao 17, na msimu wa 2016/17 alikibuka mfungaji bora kwa mabao 14, lakini akiwa sawa na Abdulrahman Mussa wa Ruvu Shooting.




Mkurugenzi Msaidizi wa Michezo wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Alex Nkenyenge (katikati), akizindua rasmi mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2021 katika Hoteli ya Slip Way jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kushoto ni Katibu Mkuu wa Kamati ya Olympiki Tanzania, Filbert Bayi, mwakilishi wa Baraza la Michezo Tanzania, Kilindi Maona, Meneja wa Bia ya Kilimanjaro Premium Lager, Irene Mutiganzi, Mkuu wa Huduma za Masoko wa Tigo, William Mpinga na Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Riadha Tanzania, Ombeni Zavala. **MPIGAPICHA WETU**

# Kilimanjaro Marathon 2021 yazinduliwa rasmi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa 19 wa mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2021, umezinduliwa jijini Dar es Salaam, huku serikali ikizimwagia sifa mbio hizo kutokana na mchango wake katika ukuaji wa sekta ya utalii na uchumi kwa ujumla.

Katika mbio hizo ambazo zinatarajiwa kufanyika Februari 28, mwakani katika Chuo Kikuu cha Ushirika mjini Moshi (MoCU), jumla ya Sh. milioni 25 zimeandaliwa kwa ajili ya washindi wa kwanza katika kila kipengele.

Akizungumza katika hafla iliyofana ya uzinduzi huo uliofanyika katika Hoteli ya Slip Way jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Msaidizi wa Michezo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Alex Nkenyenge, aliyemwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ally Possi, alisema mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zimechangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa sekta ya utalii wa michezo nchini hivyo kuchangia kuongezeka pato la fedha za kigeni.

"Tukio hili ambalo huvutia zaidi ya wageni 25,000 katika mji wa Moshi ambao baadhi yao ni washiriki na watazamaji wanaofurahia vivutio mbalimbali vya kitalii na 'kupromoti' shughuli nyingine za kiuchumi katika mji huu," alibainisha.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara si tu kuchangamkia fursa zinazoletwa na mbio hizo kwa kutengeneza faida, bali pia wahakikishe wanatoa huduma na kuuza bidhaa zenye ubora.

Aidha, alitoa wito kwa waandaaji wa mbio nyingine za marathon nchini kufuata nyayo za Kilimanjaro Marathon ambazo zimekuwa zikizingatia miongozo ya IAAF na Riadha Tanzania (RT), hivyo kusaidia kukua mwaka hadi mwaka na kuvutia wadhamini na washiriki kutoka ndani na nje ya nchi.

Kuhusu janga la ugonjwa wa COVID-19, alisema serikali itahakikisha kwamba wale wote wanaohudhuria wanapimwa, haswa wageni kutoka nje ya nchi.

"Washiriki wa mbio za Kilimanjaro Marathon hawapaswi kuwa na wasiwasi kwa kuwa tutachukua tahadhari zote muhimu katika sehemu zote za kuingilia nchini," alisema.

Aliwapongeza wadhamini wa mbio za Kilimanjaro ambao wanaongozwa na Kilimanjaro Premium Lager, wenye dhamana ya mbio za Km 42, Tigo- Km 21, Grand Malt- Km tano, pamoja na wadhamini wa meza za maji, Absa Tanzania, Unilever, TPC Limited, Tanga Cement, Kilimanjaro Water na GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel na CMC Automobiles.

Kwa upande wa Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi, ambaye pia ni Meneja wa Kinywaji cha Grand Malt, Irene Mutiganzi, alisema wanajivunia kuwa wadhamini wa mbio hizo kwa mwaka wa 19 mfululizo kwa sababu bidhaa zao hujikita kutangaza na kukuza utalii na utamaduni wa Tanzania kwa ujumla wake.

Aidha, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mbio za mwakani ambapo wametenga Sh. milioni 25 kwa ajili ya zawadi kwa washindi wa kwanza kwa mbio hizo kwa upande wa wanaume na wanawake ambapo washindi watajinyakulia Sh. milioni nne kila mmoja na kwa Mtanzania mwanaume na mwanamke wa kwanza watapata Sh. milioni 1.5 kila mmoja kama motisha.

Hivyo, amewataka washiriki kujisajili kushiriki mbio hizo kwa wakati kwani tayari usajili umeshafunguliwa rasmi kupitia njia ya mtandao wa www.kilimanjaromarathon.com a pamoja na Tigo Pesa kwa kupiga nambari *149*20# .

Naye Mkuu wa Huduma za Masoko wa Tigo, William Mpinga, alisema: "Kama kampuni ya mawasiliano inayoongoza nchini ikiwa na mtandao mpana zaidi wa 4G, tunafurahi na kujivunia kwa mara nyingine tena kudhamini Tigo Kili Half Marathon 2021 kwa mwaka wa sita mfululizo. "

## Simba, African Sports dimbani leo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wachezaji wake ambao hawajaitwa kuzitumikia timu zao za taifa wanakuwa fiti, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba watashuka dimbani leo kujipima ubavu dhidi ya African Sports ya jijini Tanga.

Mechi hiyo itapigwa leo majira saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na mwandishi wetu, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema lengo lake ni kutaka kuona kila mchezaji anakuwa katika utayari kimwili kuelekea mechi zinazowakabili za Ligi Kuu pamoja na za kimataifa.

Mbali na kukabiliwa na mechi za Ligi Kuu, Simba ina mtihani mgumu ugenini Nigeria kati ya Novemba 27-29 dhidi ya Plateau United, kwenye mechi ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Ninataka kuona kila mchezaji anakuwa tayari kwa upande wa utimamu wa kimwili kwa ajili ya kuitumikia timu katika mechi zilizopo mbele yetu," alisema.

Kwa upande wa African Sports, yenyewe inakabiliwa na mechi za kuwania kupanda Ligi Kuu wakati huu ikiwa Kundi A la michuano hiyo sambamba na African Lyon, Boma FC, GIPCO FC, Lipuli FC, Majimaji FC, Mawenzi Markert FC, Mbeya Kwanza FC, Ndanda FC na Njombe Mji FC.

## Culture Group sasa chageukia vijana

**Na Steven William, MUHEZA**

KIKUNDI cha Sanaa cha Tongwe Culture Group cha Masimba, Muheza mkoani Tanga, kimeanza kutoa elimu ya mafunzo ya sanaa kwa vijana wa miaka 10 na kuendelea kwa lengo kukuza vipaji vya sanaa na utamaduni.

Katibu wa kikundi hicho, Mohamed Levi, juzi alimwambia mwandishi wetu kuwa, ili kuenzi ngoma za sanaa na utamaduni kwa ujumla katika Wilaya ya Muheza, kikundi hicho kimeanzisha kutoa mafunzo kwa vijana wa kike na wakiume na kwamba tayari kimeshawafikia vijana 17 ambao wanajifunza kuimba, kucheza, kupiga ngoma za makabila yote bara na visiwani, kuigiza, sarakasi pamoja na michezo mbalimbali.

Aidha, Levi alisema kutokana na umaarufu na ubora wa kazi zao, kikundi hicho kimekuwa kikipata mialiko mbalimbali katika shughuli za kiserikali ikiwamo mbio za mwenge wa uhuru, viongozi wa serikali na vyama vya siasa pamoja na sherehe za watu binafsi.

Levi alisema kikundi hicho kwa sasa kinaundwa na watu 20 wakiwamo vijana 17 ambao wanapata mafunzo ya kujifunza tasnia ya sanaa za ngoma za kitamaduni na viongozi wapo watatu kati yao wakiwamo walimu wawili na mweka hazina mmoja.

Michezo
Jumatatu Novemba 16, 2020
Nipashe



RAMOS AVUNJA REKODI YA BUFFON MECHI TAIFA HABARI UK 22

KAKOSA TENA...



Beki na Nahodha wa Hispania, Sergio Ramos, akipiga penalti ambayo alishindwa kuizamisha nyavuni, hiyo ikiwa ni ya pili kuokosa katika mechi hiyo ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Uswisi wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja St. Jakob-Park jijini Basel, Uswisi. Bao la Uswisi lilifungwa na Remo Freuler dakika ya 26, kabla ya Gerard Moreno kuisawazishia Hispania dakika ya 89. **PICHA: MTANDAO**

## STARS HESABU SASA KWA TUNISIA KESHO

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kurejea juzi usiku, wakitokea Tunisia, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragije, amesema matokeo ya mechi iliyopita wameyaweka kando na kwa sasa hesabu zao ni kwenye mchezo wa marudiano utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho.

Ndayiragije amesema makosa madogo waliyoyafanya katika mechi iliyopita na kuwasababishia kufungwa bao la mapema, ndiyo yaliyowagharimu kwenye mchezo huo, lakini wataanzia pale walipoishia kesho ili kufanya vizuri.

"Nawapongeza vijana wangu kutokana na namna mechi ilivyokuwa, Tunisia ni timu kubwa, ukifanya makosa lazima uadhibiwe, ila kuelekea mechi ijayo tutaanzia pale tulipoachia.

Ninajua vijana watakuwa wamechoka kwa sababu tulianza safari saa 12 na tumefika saa tisa usiku, ila ukibeba bendera ya taifa lazima ujitolee, tumechoka lakini tumeamua kujitoa hii ni timu ya taifa kila mtu lazima ajitolee," alisema.

Ndayiragije alisema goli la mapema liliwatoa mchezoni ila kadri mechi ilivyokuwa ikiendelea waliongeza kujiamini jambo ambalo anaamini wakiwa nyumbani watajiamini zaidi na kuweza kupata matokeo katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022 nchini Cameroon.

Stars yenye pointi tatu sawa na Equatoria Guinea na Libya, ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Kundi J, huku Tunisia ikiwa kileleni na alama tisa baada ya kushinda mechi zote tatu ilizocheza hadi sasa.

# MO: CHAMA RASMI SIMBA HADI 2023

●●●Fraga, awekwa kando, atangaza usajili wa kutetemesha nchi, amkana Mukoko huku...

**Na Saada Akida**

HUKU akimtangaza rasmi kiungo wao, Mzambia Clatous Chama kuongeza mkataba wa miaka miwili ambao sasa utamalizika mwaka 2023, Mwenyekiti na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji, amesema kuanzia wiki hii, watatetemesha nchini kwa 'kutupa kombora' katika usajili wa dirisha dogo linalotarajia kufunguliwa hivi karibuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari katika ofisi zake jana, Mo Dewji alisema viongozi wa klabu hiyo hawalali na wamekuwa wakiumiza kichwa kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao katika usajili.

Alisema wameanza na kiungo wao, Chama ambaye wiki iliyopita aliongeza mkataba wa miaka miwili ambao unatarajiwa kumalizika mwaka 2023, lakini wiki ijayo watakuwa na mchakato wa usajili kwa kuziba nafasi ya Mbrazil Gerson Fraga wanayetarajia kumkosa kikosini kwa muda mrefu kutokana na kukabiliwa na majeraha.

"Suala la Chama limeisha ni mchezaji wetu halali hadi 2023, mashabiki na wanachama wa Simba wajiandae wiki ijayo tunatupa kombora letu kutafuta mbadala wa Fraga ambaye ni majeruhi.

"Tayari kuna majina ambayo kocha mkuu, Sven Vandenbroeck ametukabidhi na kuanza mchakato wa kuwapata, ila hatutayaweka wazi kwa sababu tunahofia ushindani wa klabu kubwa mfano AS Vita na Esperance ambao tumeingia katika vita moja katika usajili," alisema Mo Dewji.

Kuhusu kiungo wa Yanga, Tonombe Mukoko, alisema katika kikao chao cha bodi ya wakurugezi, hawajamzungumzia mchezaji huyo ila wanachoangalia kwa sasa ni mahitaji ya benchi la ufundi hususan wachezaji ambao wanawahitaji kuwaongezea nguvu kikosini.

Mo Dewji alisema katika suala la usajili wapo makini na hawafanyi propaganda na kuhakikisha wanawapa mikataba ya muda mrefu wachezaji ambao ni muhimu, huku akimtolea mfano Luis Miquissone waliyempa mkataba wa miaka mitatu na nusu.

"Hata kuhusu mshambuliaji wetu, Meddie Kagere, hilo litawekwa wazi kuanzia Jumanne au Jumatano ya wiki ijayo (wiki hii), pia tumewaandikia barua Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kupata ufafanuzi juu ya usajili wa wachezaji wa kigeni kuelekea Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kwa upande wetu Simba tunahitaji kuongeza nyota wawili hadi watatu ila tunasubiri kupata ufafanuzi kutoka TFF, malengo yetu ni kufanya vizuri katika michuano hiyo," alisema Mo Dewji.

Alisema mikakati yao kwenye Ligi ya Mabingwa ni kufanya vizuri na kufika nusu fainali na kwamba wametenga bajeti nzuri ikiwamo usajili wa nyota hao, mahitaji muhimu ya timu pamoja na motisha kwa wachezaji wao ili kufanya vizuri.

"Msimu huu malengo yetu ni kutetea ubingwa, hivyo tuna imani ya kufanya hivyo, kuteleza kidogo haitaturudisha nyuma, pia Ligi ya Mabingwa kufanya vizuri na kutorudia makosa ya msimu uliopita kutolewa katika hatua za awali," alisema Dewji.

Alisema ana imani katika michuano ya kimataifa kuna mambo mengi ambayo yana faida na hasara, lakini kwa upande wa Simba watafaidika kucheza mechi ya awali bila ya mashabiki ugenini dhidi ya Plateau United ya Nigeria, huku watakaporudiana hapa nchini mashabiki wakiruhusiwa.

"Hivi karibuni CAF imeruhusu mchezo wetu wa marudiano kati ya Taifa Stars na ya Tunisia mashabiki asilimia 50 kuingia uwanjani kushuhudia mechi, kwa sababu Tanzania hakuna corona, hii pia ni nzuri kwa Simba kwa kuwa mechi ya marudiano tutacheza mbele ya mashabiki wetu," alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu kushikiliwa kwa Hashim Mbanga pamoja na kuitwa Polisi kuhojiwa kwa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa, Mo alisema suala hilo lipo chini ya kisheria hivyo hataweza kulizungumzia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002